Ufunuo, Mlango Wa Nne Sehemu Ya II

Furaha sana kuwa humu tena asubuhi ya leo. Nilikuwa tu nikifikiria jinsi ambavyo theluji hii. . .Sasa, na kama tungalikuwa Colorado, theluji hii ingekuwa nyororo sana na yenye manyoya, na iwe kama arobaini chini ya sufuri. Nawe ungeninii "Fuu. . ." ungeipulizia namna hiyo, na kuingia moja kwa moja mavumbini. Na ingekuwa jinsi hiyo kwenye msimu wote wa baridi kali. Lakini sasa, kama ilivyo hapa, kwenye hii ninii. . .kwa namna fulani katikati, katikati ya maeneo, sasa inakuwa majimaji sana na yenye matope na mbaya, na—na inaonekana tu kama kwamba la—laiti ningaliruka, niende huko Arizona, na kungoja mpaka msimu wa kuchipusha kisha nirudi.

2 Hivyo ndivyo sisi sote hupata mafua, viini na kadhalika sasa viko ardhini na vitaganda kisha viyeyuke, halafu vigande kisha viyeyuke. Na hiyo hupanda juu nasi tunaivuta ndani, ndipo tunapata maumivu ya koo, kuumwa na kichwa, na maumivu na uchungu. Na, jamani, jamani, ni wakati wa jinsi gani, ni mahali pa jinsi gani.

> Bali kuna nchi ng'ambo ya mto,
> Wanayoita hiyo tamu milele,
> Na tunaifikia tu pwani hiyo kwa mkataa wa imani;
> Moja kwa moja tutafika kwenye hilo lango,
> Pale tukaishi pamoja na wasiopatikana na mauti,
> Siku moja watapiga hizo kengele za dhahabu kwa ajili yako na yangu.

3 Huko ndiko tunakoenda Nyumbani kukaa basi, sivyo? Hiyo ndiyo siku tunayoitazamia.

4 Sasa, jana usiku hakika nilifurahia hayo mahubiri ya ajabu na kadhalika niliyosikia kutoka kwa ndugu zangu. Yuko wapi Pat Tyler, je, yuko ndani asubuhi ya leo? Pat, loo, sikukuona umeketi papo hapo mkubwa kama uhai na wa asili maradufu. Na—na si—sikukuona umeketi hapo. Mara ya kwanza nilipokuwa na Pat. . .nilipomsikia Pat akizungumza; bila shaka nilifurahia hayo, nina hakika sote tuliyafurahia.

5 Halafu basi maskini ndugu aliyetoa ule ushuhuda motomoto wa mahubiri hapa ambaye kweli alisikika kama bombomu ikirusha risasi. Ndugu fulani, nilikutana naye, kutoka Ohio. Yuko hapa asubuhi ya leo? Mahali fulani hapa? Ndugu Neville alitoa sifa zake kwamba yeye huzungumza kwa kasi sana.

6 Halafu Ndugu J. T. Parnell. Na—nami nadhani kamwe hawakumfikia Ndugu Beeler. Naye, Ndugu Parnell, yuko hapa? Ndugu Parnell, Ndugu Beeler? Sina hakika, nilidhani nilimwona Ndugu Beeler.

7 Taa hizi, hii ni ninii. . .Wakati watakapoijenga maskani mpya, natumaini ya kwamba wataifanya tofauti, tofauti kidogo. Hii ndiyo yetu ya kwanza, ya majaribio. Na kwa hiyo tukiwahi kupata nyingine, mbona, tunataka iwe tofauti kidogo na hii; huwezi kuona; ningependa maskani kwa namna fulani ijengwe ikiinama chini namna *hii*, wasikilizaji. Unaangalia moja kwa moja kwenye wasikilizaji wako wakati wote. Na hasa sana kwenye mikutano ya upambanuzi, unaweza tu kuzunguka moja kwa moja. Mnaona, uwataje moja kwa moja namna hii, moja kwa moja huku na huku. Halafu basi, hata kama una roshani ndogo ya kutokea, ni bora zaidi.

8 Ndugu Littlefield, kama Billy yuko hapa, alinipigia simu jana usiku naye anatuma sifa za ile maskani niliyoweka wakfu kule, ambayo wasanifu majengo. . .Ndugu Wood, iligharimu, naamini, dola mia tano kwa msanifu majengo kuichora tu. Naye a—anatuma hizo pamoja na bei na kila kitu cha nyenzo zote na kila mbili-kwa-nne na ninii kwa ninii zinazoambatana nayo. Na anatutumia, na anataka kuja; naye alisema angeenda kwa watu wa mbao na kadhalika aone kama hawezi kuwafanya wafanye m—mkato kama walivyofanya kwa yake. Maskani ya kupendeza sana, si kubwa sana, bali ni mjengo mzuri.

9 Kwa hiyo nilimwambia, nikasema, “Ni—nitawapa huo wadhamini na mashemasi mara utakapomtumia Billy na—na ndipo tutaacha waone makadirio ya kiasi walicho nacho cha kuanza ujenzi wao.”

10 Akasema, “Mkifanya hivyo, mimi naja, nivae jozi ya ovaroli na kukaa tu pamoja nanyi kwenye wakati huo.” Ndugu Littlefield ni mtu mzuri, mtu mpendwa, mzuri sana.

11 Sasa, je, nyote mnajisikia mko tayari kabisa, kuanza Mwaka Mpya sasa? Amina! Tuingie moja kwa moja kwenye Mwaka Mpya. Tunataka kuuanza vizuri, tukimtumikia Bwana. Ni wangapi walioamka asubuhi ya leo na kumshukuru Yeye kwa ajili ya mwaka uliopita na yote uliomaanisha, na kumwomba, “Sahau yaliyopita”? Kwa hiyo, tulifanya hivyo kando ya kitanda tulipoamka, kisha tukaja mezani na ambapo kwa kawaida maskini madhabahu ya familia, wanakusanyika mezani na kuomba.

12 Na kwa hiyo daima sisi hujaribu kuwa na tabia ya kuomba usiku kabla hatujaenda kulala. Ninayo, hiyo, tangu nilipoongoka. Ninaamka asubuhi, na kuna giza sana na ukungu mno nisingeweza kutembea, si—sijui ninakoenda. Bali nikimwomba tu aushike mkono wangu na kuniongoza siku nzima.

13 Ndipo ninakumbuka, moja kwa moja upande wa pili wa barabara hapa, nilipokuwa tu kijana, Billy Paul alikuwa na umri wa miaka mitatu hivi, ama minne, nasi tuliishi ng'ambo tu ya barabara. Basi usiku mmoja alitaka maji ya kunywa, nayo yalikuwa huko jikoni, kichoteo katika ndoo. Nami nikasema . . . Loo, nilikuwa nimechoka sana, nilikuwa nimefanya kazi kwa bidii siku nzima na kuhubiri nusu usiku. Na—naye akasema, "Baba, na—nataka maji ya kunywa."

14 Nami nikasema, "Billy, nenda moja kwa moja jikoni pale, yako kwenye ile meza ndogo." Nikasema . . .

15 Akaamka, akapangusa macho yake, na kuangalia kule, akasema, "Baba, ninaogopa kwenda." Mnaona?

16 Nami nikasema, "Vema, hiyo ni . . . ni sawa." Nikasema, "Hima, kipenzi, ukanywe maji. Baba ni mchovu sana." Umbali kidogo tu, kama kufika kwenye lile dirisha.

Ndipo a—akasema, "Lakini ninaogopa kwenda, baba." Mnaona?

17 Vema, nikaamka na jamaa huyo mdogo. Naye akaushika mkono wangu, na lilikuwa ni jambo zuri; hatukuwa tumeenda hatua nne ama tano kabla hajajikwaa kwenye zulia ambapo Meda alikuwa ametia nta sakafuni, na juu ya kipande cha zulia la plastiki, nanyi mnajua jinsi hiyo ilivyo. Naye akateleza sana, bali nilikuwa nimeushika mkono wake, halafu naye akanishika tu kwa nguvu zaidi. Ndipo nikasimama pale kidogo, na kuwazia, "Mungu, hiyo ni kweli." Mnaona? "Sitaki kupiga hatua moja bila ya Wewe kuushika mkono wangu, maana sijui ni wakati gani nitakapoteleza." Mnaona? "Na maadamu tu ninaweza kuuhisi huo mkono Wako mkubwa, wenye nguvu ukiushika wangu, ninajua Wewe utanishikilia wakati wa ninii yangu . . . " Mnaona?

18 Kwa hiyo mimi hujaribu kufanya mazoea ya hilo, ku—kuuweka mkono wangu katika Wake. Na wakati mwingine nimefanya mambo ambayo yanaonekana ya dhihaka machoni pangu, mambo yanayoonekana yasiyo ya kawaida kwa akili ya mwanadamu; bali tukiyaachilia tu, ninakuta kwamba ndilo jambo pekee lingeweza kufanywa ili kuwa sahihi.

19 Mnajua, mambo ambayo hayaonekani ni sahihi hapa, kama Mungu akikuongoza kwake, yatakuwa sahihi hapa nje mahali fulani, unaona, maana Yeye anajua jinsi ya kuongoza. Kwa hiyo, tukiona kwamba Yeye ndiye neema yetu itoshelezayo kwa yote, na yote tunayohitaji ama kuyajali ni Yeye, basi na tuweke kando kila kitu ila Yeye na kuushika mkono wa Mungu usiobadilika.

20 Tulikuwa tukiimba wimbo hapa, sijausikia ukiimbwa kwa muda mrefu. Sasa, siwezi kuimba na hapa kuna ninii . . . Sidhani kuna wageni wowote pamoja nasi. Kwa hiyo mimi . . . Hiyo ndiyo sababu ninajaribu maskini nyimbo hizi, mwajua, maana ninazipenda tu. Nawe Gene, ukiachilia hii itoke kwa njia ya

kanda hii iende kwa umma . . . Tulizoea kuimba maskini wimbo mdogo hapa:

Wakati umejaa fasiri za haraka,
Hakuna kitu kisichoweza kusogezwa duniani.
Jenga matumaini yako juu ya vitu vya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Ni wangapi mliowahi kuusikia wimbo huo? Loo, naupenda, nanyi je? Hebu tujaribu kifungu chake:

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya vitu vya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Hebu tujaribu kifungu kimoja:

Safari yetu itakapomalizika,
Na tumekuwa waaminifu kwa Mungu,
Makao yako mazuri na yenye kung'aa ya Utukufuni,
Nafsi yako iliyojaa furaha itayaona!

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya vitu vya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

21 Hebu tusimame sasa kwa dakika moja tu kwa maombi, mkipenda, tunapoinua mmoja wa mikono yetu kwa Mungu na kuuimba huo tena:

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya vitu vya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

[Ndugu Branham anavumisha—Mh.]

. . . -tamani utajiri wa bure wa dunia hii,
Ambao unaoza upesi sana,
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Hayatapita kamwe!

22 Baba wa Mbinguni, tunaposimama, Bwana, tunapenda tu kuziimba nyimbo hizo za kale, hizo huingia ndani katika sehemu za ndani sana za moyo wetu na kuonyesha upendo wetu Kwako, Mungu aliye hai. Na wakati tulipoinua mikono yetu, Bwana, asubuhi ya leo, ilikuwa ni kumbukumbu ndogo ambayo "Ishike mikono yetu, Bwana." Kama nilivyokuwa nikisimulia juu ya Billy Paul, jinsi ambavyo aliushika mkono wangu kwa nguvu, angalianguka kama isingalikuwa kwamba nilikuwa nimemshika. Pia, Ee Mungu, ni mara ngapi tungalikuwa tumeanguka kama haikuwa kwamba Wewe uliushika mkono wetu! Nikiwazia jinsi ambavyo yeye, akiwa hana mama, kama mtoto mchanga . . . na jinsi ambavyo . . . jinsi ambavyo kote

katika maisha, kwamba njia alizokuwa amepitia, angalikuwa ameuawa muda mrefu uliopita, bali kulikuwako na Mkono mkuu ambao ungeweza kufika ambapo wangu usingeweza kufikia, na kumshika. Sasa, tunashukuru sana kwa jambo hilo.

23 Nina furaha sana kujua, Bwana, ya kwamba tunapoisikia nafsi yetu ikitengana na mwili huu, ya kwamba kungali na mkono ambao tunaweza kuuendea na kuushika, utakaotuongoza kuuvuka ule mto. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya mambo haya, hakikisho hili, hakikisho hili lenye baraka tulilo nalo, Nanga ya nafsi, inayotuweka imara tunapotembea kwenye safari hii ama kuiabiri bahari wazi ya maisha yenye huzuni.

24 Nasi tunaomba, Baba, kwamba kama alivyosema yule mshairi, "Ndugu mpweke, aliyepatwa na ajali ya meli, akiona uimara wetu (tumetulia), akiona hivyo, atatiwa moyo tena, ama kujipa moyo tena na kujaribu tena"; ajue ya kwamba Mungu atoshelezaye kwa yote, kama tukijikwaa au kuanguka, mkono Wake mkuu upo kutusaidia. Neema Yake yatosha.

25 Sasa tunaomba, Mungu, ya kwamba, asubuhi ya leo, tutaanza Mwaka Mpya katika nyimbo na kuimba na kushangilia, na tukijua ya kwamba Mungu atatuongoza kote katika safari ya maisha na kuuvuka mto wa mauti, tuingie kwenye Nchi hiyo ya ahadi. Macho yetu yanaangalia ng'ambo ya vijito vilivyofurika vya Yordani asubuhi ya leo, ambako mashamba ya—ya majani matamu na mashamba ya majani yasiyokauka yanakua, nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba nafsi zetu zitalishika ono hilo na kamwe zisiachilie. Siku moja tutakapolazimika kuja kwenye kijito hicho mahali kinapokingama, ambapo, kama Eliya wa kale, Vazi la Mungu litavipiga vijito vya mauti nasi tutatembea tuvuke bila hofu. Tujalie, Bwana.

26 Tusaidie tunapolikaribia Neno Lako. Ee Bwana, ninaomba ya kwamba Roho Wako Mtakatifu atalitia mafuta Neno hili. Hakika hatutoshi kuyafundisha, kwa kuwa si mwalimu. Tunajua ya kwamba njia pekee tutakayoweza kulijua ni yule Mwalimu mkuu aje na kuchukua makazi Yake—Yake mioyoni mwetu, na—na kuzitawala nia zetu hivi kwamba (na mawazo yetu) mpaka tutaninii . . . Yeye atatufasiria Maandiko Matakatifu. Tunategemea hilo kwa uchaji. Basi liwazie hilo, Mungu.

27 Loo, jinsi inavyopendeza sana kwamba Baba aliye hai jinsi hiyo, aliyekuwa tangu . . . ambaye ndiye chanzo hasa cha Umilele, ambaye angewashukia wanadamu na kutusaidia, na angeleta Neno Lake na kulitoa kwa vinywa vyetu na mioyo yetu na masikio yetu ili tuweze kulisikia na kuishi, lipate kutukomboa na laana ambayo hatukuhusika na kuja kwake, Baba, kwa sababu ilifanywa na jamii ya binadamu nasi ni uzao wa huyo—huyo mume na mke wa kwanza. "Nasi tumezaliwa katika dhambi, tukaumbika katika uovu." Bali Mungu mwenye haki na aliye hai anajua ya kwamba hatukuuchangia huo, bali

amefanya njia ya kuepukia na kutupa majaliwa ya kuja. Jinsi tulivyo na furaha tumekuja katika Nyumba ya Baba!

28 Tunaomba sasa, ya kwamba utalibariki kanisa letu hapa, Ndugu Neville, mchungaji we—wetu hodari, mtumishi Wako mnyenyekevu. Tunawaombea mashemasi wetu na wadhamini wetu, ya kwamba utawapa mwaka ulio mkuu kuliko yote waliyowahi kuwa nayo. Tujalie, Bwana. Wape maisha marefu. Watie nguvu, bwana, hao ni watumishi Wako. Jalia daima wakae kishujaa kwenye wajibu wao. Wabariki walei, wa—washiriki, watoto Wako wapendwa wanaokuja kwenye nyumba hii. Mungu, tunaidai nafsi ya kila mmoja wao anayeingia nyumba hii. Tunawadai kwa ajili Yako, Bwana. Tusaidie tuwe wahudumu wazuri sana ambao watalileta Neno kwa urahisi na ukweli sana, kwa Roho Mtakatifu, hata watatamani kuwa kama Wewe, Bwana. Tujalie. Waponye wagonjwa na wanaoteseka ambao huingia. Na kote ulimwenguni, lijalie katika kila nyumba ya Mungu.

29 Hatimaye, utakapomaliza, Bwana, jalia tuingie kwenye malango Yako, tukaketi kwenye meza ya makaribisho ya Mungu, na tule na tuishi pamoja katika nyakati zisizo na mwisho. Hadi wakati huo, jalia tuwe na afya na nguvu, furaha, shangwe, nguvu na uweza, na baraka za Roho Mtakatifu zituongoze. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina. Mwaweza kuketi.

30 Nimeufurahia uimbaji huo mzuri asubuhi ya leo. Ambapo. . .Niliingia tu, katika wakati mzuri, nikizungumza na rafiki yangu msiri, Ndugu Skaggs, na—na Ndugu Gene huko nyuma, na ndugu mwingine mlangoni; mpaka nikapata kusikia sehemu yake, lakini ilikuwa ikitokea kwenye kinasasauti vizuri sana.

31 Ninyi nyote mnaufurahiaje Ufunuo? Vema? Ninaamini sana kama msichana wangu mdogo, Sarah, huko nyuma, imekuwa ni "mapinduzi" kwangu mimi, ni—ni mapinduzi tu yakiendelea zaidi na zaidi. Mnajua, laiti tungalikuwa tu na wakati sasa hadi yapata Machi ama Aprili, tuweke tu turubai kubwa huku nyuma na tushuke tuje tu mchana na kuzichora picha hizo na chati nzima, na kuziinua tu juu na chini kama vizibo vya madirisha, mwajua, kama vile sikuzote nimeota juu ya kuwa na maskani kubwa mno mahali fulani ambapo ningenyosha mkono na kushusha chati hii, ishuke mpaka jukwaani; na funuo na fasiri Bwana alizonipa, na kuchukua kijiti na kuanzia pale na kuzishusha nyakati hizi zote. Ndipo tukimaliza hayo, tuinue hiyo, kisha tuishushe hiyo nyingine namna *hii* na kuanza na hiyo, na kuifundisha yote. Loo, hiyo ingekuwa tu ni kama mbingu ndogo, sivyo? Tuketi tu kwenye msimu wote wa baridi kali, tuketi tu pamoja na Bwana.

32 Ni vema sana kuwa peke yako na Yeye! Mwajua, tulizoea kuimba wimbo, "Zipo nyakati ninazopenda kuwa peke yangu

pamoja na Kristo Bwana wangu, ninaweza kumwambia shida zangu zote peke yangu.” Mnaona, ndivyo unavyopaswa kuwa. Walizoea kuimba, Roy Davis, alizoea kuimba wimbo mdogo, *Nenda Kisiri Ukaombe pamoja na Yesu.* Kila kitu kinaelekeza tu. . .kila kitu unachoweza kuangalia daima hurudi moja kwa moja kwenye mstari wa Yesu Kristo, sivyo?

33 Sasa, kwenye nyakati za kanisa tulizonena habari zake, siku nane zilizopita mkutanoni. . .Halafu jana usiku nafikiri tulifikia kwenye kifungu cha pili cha mlango wa 4 wa Ufunuo. Nami nadhani ninyi nyote mlikuwa hapa jana usiku ku— kulipata. Na kwa hiyo mimi. . .labda kama nikifika kwenye kifungu kimoja ama viwili vyake asubuhi ya leo, na. . . Ama umbali ule Bwana atakaoongoza, sijui. Nimefikia yapata kifungu cha 6 ama cha 7 hapa, kifungu kidogo tu kilichoandikwa hapa ambapo ninaweza kurejea katika sehemu mbali mbali za Maandiko na kutoa mambo hayo, na mahali niliposoma jana.

34 Na sasa, tunaona, tuliachia jana usiku, ninaamini, kwenye kifungu cha pili, kuanzia cha 3, nafikiri ndipo. Nasi tuliachia tu kwenye “Sauti ya Parapanda.” Hiyo si ni kweli, “Kutolewa kwa Sauti”? Hebu nikisome chote tupate kukirejea sasa:

> *Baada ya haya naliona, na tazama, mlango ukafunguka mbinguni: na sauti ile ya kwanza niliyoisikia* ilikuwa *kama sauti ya baragumu ikinena nami; ikisema, Panda hata huku juu, nami nitakuonyesha mambo. . .hayana budi kuwako baada ya hayo.*
>
> *Na mara nalikuwa katika Roho: na tazama, kiti cha enzi kimewekwa mbinguni na mmoja ameketi juu ya kile kiti.*
>
> *Na yeye aliyeketi kwenye* kiti cha enzi. . .*yeye aliyeketi alionekana mithili ya. . .jiwe la yaspi na. . . akiki: na upinde wa mvua ulikizunguka kile kiti cha enzi,* ukionekana *mithili ya zumaridi.*

35 Sasa, somo hili zuri, loo, zuri! Na asubuhi ya leo, kabla tu sijashuka kuja huku, nilifikia hapa chini kwenye kifungu cha 6, nikawazia, “Loo, jamani, siwezi kupita hapo, kwa kuwa hiki hapa kitu fulani kwenye kifungu hiki cha 6 ninataka watu wote wasikilize vizuri sana, tutakapofika kwenye *wanyama* hawa.” Ufafanuzi mbalimbali wa wanyama hawa hapa, tukirejea kwenye ya asili, mmoja ni aina moja ya mnyama, na hao wanyama wengine wanne ni aina nyingine. Mmoja ni mnyama, katika Kiyunani, kama “mnyama mwitu.” Huyu mwingine hajafasiriwa vizuri katika toleo la King James, kwa kuwa si *wanyama*, ni “Viumbe hai.” Na jinsi ambavyo hao Viumbe, kile walichokuwa, hawakuwa wanadamu wala hawakuwa Malaika. Kwa hiyo ni “Viumbe hai,” na jinsi ambavyo walikuwa na nyuso nne na ninii nne. . .Loo, jamani, tutayaleta hayo moja kwa moja

kwenye Injili, na kuyarejesha moja kwa moja na kuyaweka leo kikamilifu kama ilivyo hapa. Pia, kumbukeni, *nne* ni namba ya duniani. Mnaona? Na ni somo zuri tu pale, na kwa hiyo ni—nina hakika kabisa hatutayafikia hayo; labda tutayafikia. Lakini ni mazuri sana!

36 Halafu, Bwana akipenda, ndipo kama tuko huku, labda Jumapili ijayo huenda tukajaribu hilo tena; tujaribu, chini, tuone kama tunaweza kuumalizia mlango huu wa nne kabla hatujaondoka. Bado hatujui mahali hasa tutakapoanzia.

37 Sasa, tunaona ya kwamba *baada*, "Baada ya mambo haya." *Baada* ilimaanisha "Baada ya nyakati za kanisa kwisha."

38 Ndipo Yohana aliitwa apande juu zaidi, "panda hata huku juu," ambalo linamaanisha "panda huku juu." Alimwonyesha yote yaliyokuwa yanaenda kutendeka katika ulimwengu wa—wa wakati wa Kanisa. Ndipo baada ya nyakati za kanisa kwisha, tunaona basi ya kwamba Yohana alikuwa ni mfano wa kila mwaminio wa kweli ambaye ataitwa na Kristo apande Juu. Hiyo ni kweli? Kuitwa, "Panda huku juu."

39 Nasi tunaona ya kwamba Sauti iliyosema naye ilikuwa ni Sauti ya baragumu, dhahiri, wazi, nayo ilikuwa ni Sauti ile ile iliyonena naye hapa duniani. Mnaona, maadamu Yeye alikuwa katikati ya vile vinara saba vya taa vya dhahabu, Yeye alikuwa akizungumza na . . . ama *kutoka*. Loo, ninapenda hilo, "akinena kutoka kwenye vinara vya taa." Mnaona, Yeye alikuwa kwenye vile vinara vya taa, akinena kutoka humo kwa Kanisa Lake. Ndipo hapo wakati wa kanisa ulipokuwa umekwisha, Yeye aliondoka duniani na kupaa juu Mbinguni ndipo akawaita watu Wake Waliokombolewa wapande juu pamoja Naye. Loo, hilo si ni zuri? Ni—ni . . . Loo, linaufanya tu moyo wangu kuruka.

40 Basi kumbukeni, tunapovileta vitu hivi, ninawatakeni hasa sana waongofu wachanga kama Dada Ina hapa, ama, na Ina, hasa, na mumewe, na Rodney na—na mkewe, na Charlie na hao wengine, waelewe ya kwamba mambo haya, na wengi wenu vijana ambao ndio kwanza mwingie kwa Bwana, ambao hamjafika mbali sana safarini bado, mmemwonja tu na kuona kwamba Yeye ni mwema na mwenye neema. Sasa, angalieni jambo hili, ya kwamba mambo haya tunayonena habari zake, kile tunachojaribu kufanya ni kuiimarisha Imani yenu, ya kwamba Mungu anaposema jambo lolote halina budi kutukia. Kamwe halitashindwa! Haidhuru . . . Huenda likaonekana kana kwamba ni maili milioni moja . . . wala haliwezi kutukia, bali Mungu atalisukuma huku na huku na kulifanya litukie. Naye hufanya hivyo kukujaribu.

41 Angalia yale aliyomwambia Ibrahimu. "Mpeleke mwanao hapa juu ya kilima ukamwue," akiisha kumgojea kwa muda wa miaka ishirini na mitano. Naye akasema, "Mpandishe hapa ukamwue." Na vipi . . . ? "Nitakufanya baba wa mataifa."

42 Naye Ibrahimu, umri wa miaka mia moja; mke wake, tisini; na mtoto wao wa pekee. . .Ibrahimu alikuwa na yapata umri wa miaka mia moja na kumi na mitano wakati huo. Kwa hiyo akasema, "Yeye atakuwaje, i—inawezekanaje? Ikiwa mimi, mzee, kadiri nilivyozeeka, na nilingojea kwa muda wa miaka ishirini na mitano. . .Ulinipa ahadi hiyo kwenye umri wa miaka sabini na mitano, nami hapa nina mia moja. Naye Sara alikuwa na sitini na mitano, na sasa ana tisini. Vipi? Tukiisha kumpata mtoto huyu. . .Na Wewe uliniambia huko nyuma kabisa, miaka ishirini na mitano iliyopita wakati nikiwa na miaka sabini na mitano, 'nitampata mtoto' baada ya kuishi na Sara miaka hii yote, nilikuwa mgumba naye tasa. Kwa hiyo vipi? Isitoshe, uliniondolea ugumba na ukamwondolea utasa, kisha ukaja ukatupatia mtoto huyu. Nasi tumemlea hapa akafikia umri wa miaka kumi na mitano, na kupitia kwa mtoto huyu ulisema Wewe 'Ungeyabariki Mataifa na kila taifa ulimwenguni,' na kunifanya baba hata wa Mataifa, kunifanya baba. Ndipo katika nyakati zijazo, Bwana, ya kwamba Wewe utanifanya baba wa kila taifa chini ya mbingu kupitia kwa mtoto huyu. Na kupitia kwa mtoto huyu angekuja Mkombozi, na kupitia kwa Mkombozi huyo angekomboa jamii yote ya binadamu. Utafanyaje jambo hilo, Bwana?" Hayo hayakuwa mawazo ya Ibrahimu, hilo halikuwa swali la Ibrahimu. Utii! Hakusema, "Utafanyaje jambo hilo?"

43 "Si kazi yangu. Ulisema hivyo, kwa hiyo ninajua Neno Lako ni la kweli, ikiwa unaweza kulitimiza Neno Lako kwangu na unaweza kunionyesha ya kwamba nilipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano; wakati uliponiita na kusema, 'Jitenge na usafiri uende katika nchi ya kigeni,' nimekuwa katika nchi hii kwa muda wa miaka ishirini na mitano. Niliondoka, mzee, nikiishi na mke ambaye nimeishi naye tangu alipokuwa msichana," yeye akiwa ni dada yangu wa kambo. "Kisha nikai-. . .wakati huu wote. Na Wewe ulinipa mtoto huyu uliyeahidi; nilimpokea kama mtu aliyetoka katika wafu. Na kama ukisema 'mwue,' Wewe unaweza kumfufua katika wafu tena." Loo, jamani! Hivyo ndivyo, jambo ndilo hilo. Naye alifanya hivyo.

44 Na mara alipomtii Mungu katika ukamilifu, akaondoa nywele za Isaka kutoka usoni mwake, akachomoa upanga amwue. . .mwanawe mwenyewe, mwanawe wa pekee. Mungu alikuwa akionyesha mfano, akituonyesha. Kwa nini akafanya hivyo? Haikumbidi kufanya hivyo. Bali alilifanya kusudi mimi na wewe, tupate kuangalia mambo haya katika siku hizi za kuogofya zenye giza ambapo mioyo ya wanadamu imejaa sana maovu, tuweze kujua ya kwamba Mungu hutimiza ahadi Yake. Haidhuru linaonekana halitoshi jinsi gani, jinsi ambavyo huenda haliwezekani, Mungu angali anadumu Mungu na hutimiza kila ahadi aliyotoa.

45 Hilo ndilo ninalojaribu kuwaambia tunaposimama hapa kwenye ibada ya uponyaji. Kusimama hapa, unasema, "Mimi ni mgonjwa." Nawe. . .Hiyo hapana shaka, wewe ni mgonjwa. Lakini Mungu hutimiza ahadi Yake! Ndipo atashuka. Sasa, unaona, Yeye alifanya upatanisho hapa kwamba Yeye—kwamba Yeye atakuponya. Hivyo ndivyo Yeye alivyofanya. Sasa, jambo pekee analokuomba ufanye ni kuamini hilo, lishikilie tu kama vile Ibrahimu alivyofanya.

46 "Vema, daktari anasema ni—nitaishi siku moja zaidi."

47 Sijali. Hilo ni sawa, hayo tu ndiyo mtu huyo ajuayo, hivyo ndivyo vizuri zaidi ajuavyo. Ibrahimu angempokeaje mtoto huyu akiisha kumweka pale juu, nalo Neno la Mungu lilimwambia "nenda kamwue huyo mvulana"? Atafanyaje hilo? Hilo silo swali. Mungu alisema ufanye hivyo na hilo latosha. "Nitapataje kupona na daktari anasema ya kwamba siwezi kupona?" Mimi. . .hiyo si ninii yangu. . .si langu kupigia swali; ni kuchukua Neno la Mungu. Na mara hilo likifunuliwa kwako ya kwamba utapata afya, basi wewe—wewe kumbuka tu utapona. Hakuna kitu kinachoweza kukuzuia. Hiyo ni kweli. Unaona?

48 Kwa hiyo wakati Ibrahimu akiwa katika utii mkamilifu. . . Atafanyaje hilo? Dakika za mwisho, dakika tano za mwisho zikaja, dakika tatu za mwisho, dakika mbili za mwisho, dakika moja ya mwisho, sekunde thelathini za mwisho, sekunde ya mwisho ikafika, wakati mkono ulikuwa tayari umeinuliwa juu kuyaondoa maisha ya mvulana huyo, Mungu alisema, "Achilia papo hapo. Achilia papo hapo, unaona. Ninaona kwamba kweli wewe unanitumainia. Sasa, ndio kwanza nifanye hivi, Ibrahimu, kuionyesha maskani ya Branham katika siku zijazo, unaona, kile kinachoendelea, kwamba hawana budi kunitumainia Mimi. Hawapaswi kunishuku hata kidogo. Wanitumainie Mimi!"

49 Karibu wakati huo, yeye. . .Hii hapa sadaka, hakuifanya bure. La, hakuifanya bure, kwa kuwa mara mwa—mwana-kondoo akalia, maskini kondoo dume alikuwa amenaswa kule nyikani kwa pembe zake. Na ni mara ngapi tumepitia hayo. Je, huyo kondoo dume alifikaje huko? Vipi, kupitia kwa wanyama wote wa mwitu? Maili mia moja kutoka kwenye ustaarabu, miongoni mwa simba, mbweha, mbwa mwitu, kila namna ya mnyama mwitu huko nyuma, huko juu kabisa mlimani ambako hakuna maji wala nyasi, alikuwa akifanya nini kule? Mungu alimuumba, akamweka tu pale.

50 Na kumwona katika siku zetu tunazoishi! Sasa, asubuhi ya leo itanibidi kufanya kwa wingi sana ma—mambo ya kibinafsi kulisema, kufikia yale ninayotaka kusema. Hiyo ndiyo sababu ninaliwekea hili msingi jinsi ninavyofanya, kabla ya kuanza haya. Ninawatakeni mwelewe kwamba mambo haya yanayosikika ya kibinafsi, hayakusudiwi kuwa ya kibinafsi.

Yanaletwa tu kutoa mfano kwenu kusudi imani yenu itulie kwa uchaji katika imani iliyo katika Kristo, mpate kutulia juu ya ahadi Yake. Maana Mungu hutimiza ahadi Yake kikamilifu tu iwezekanavyo, sasa akituonyesha.

51 Na hebu mwangalieni *Yehova-yire* lilo hilo, ambalo Ibrahimu alimwita, ambalo katika Kiebrania linamaanisha "Mungu atajitolea Mwenyewe sadaka." Mungu anaweza kufanya hivyo. Alifanya njia Yake. Kama Yeye alisema . . . Alimwambia Nuhu . . .

52 Ulisema, "Vema, hiyo ilikuwa ni Ibrahimu tu." La. Yeye alisema kote katika wakati, na angali anasema.

53 Alimwambia Nuhu huko nyuma, kwamba, kama tunavyoliendea asubuhi ya leo, "Mbona, itanyesha." Mbona hakukuwako . . . kamwe hakukuwahi kuwa na wingu angani. Kijito kikubwa kuliko vyote cha maji kilikuwa ni mkondo ambapo Mungu aliinyunyizia nchi maji, chemchemi ndogo mahali fulani. Hicho kilikuwa ndicho kijito kikubwa kuliko vyote cha maji kilichokuwapo.

54 Sasa, watu wanasema, "Kutatokeaje maji yoyote kamwe huko juu? Nionyeshe mahali yalipo huko juu kwenye lile jua lote lenye joto, kama hakuna yoyote kule juu."

55 "Kama Mungu alisema, 'jenga safina, kwamba hiyo inakuja,' ni jukumu langu kuijenga safina na kujiweka tayari, maana inakuja. Yeye ni Yehova-yire, anaweza kuweka maji huko juu."

56 Na jambo pekee alilofanya ni kumwacha mtu, mtu mjinga, mpumbavu, afanye hasa kwa sayansi yake, kuyatimiza yale aliyojua yangekuja. Mungu kamwe hakuuangamiza ulimwengu; mwanadamu huangamiza ulimwengu. Mungu haangamizi chochote, Mungu hujaribu kuhifadhi kila kitu. Mwanadamu hujiangamiza mwenyewe kwa maarifa yake, kama alivyofanya katika bustani ya Edeni kwenye ule mti, na kadhalika. Na kwa hiyo mwendawazimu fulani alishika nguvu fulani za atomiki, mahali fulani, walizokuwa nazo.

57 Wa—wangeweza kufanya kazi nazo basi, maana wangeweza kufanya mambo nazo wakati huo ambayo kamwe hatujawahi kujifunza bado. Hatujaendelea mbele jinsi hiyo. Labda itachukua miaka mitatu ama minne bado, ama zaidi, kabla hatujaweza kuyafanya, kufanya yale waliyofanya. Walijenga piramidi na sfiniksi na kadhalika. Tusingeweza kufanya hivyo kamwe. Tusingeweza kufanya hivyo, hakuna njia ya sisi kufanya hivyo, isipokuwa tu tukiweza kupata nguvu za atomiki. Nguvu za petroli, nguvu za umeme, zisingeweza kuinua moja ya majabali hayo, zisingeweza kuyanyanyua toka ardhini. Na mengine yana urefu wa jengo la mji, juu hewani, na yakiwa na uzito wa tani bilioni moja. Waliyanyanyuaje huko juu? Mnaona, walijua.

58 Nao wakaachilia hayo, mtu fulani akaachilia moja ya hayo mabomu ya atomiki liruke kwenye skrini ya mwingine, huko nyuma katika siku hizo. Maana, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, kama ilivyokuwa, ustaarabu wa aina hiyo, aina hiyo ya watu werevu; kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Marudio ya jinsi ilivyokuwa! Mnaona?

59 Hapa muda si mrefu uliopita walichimbua mfumo wa kisasa wa ugavi wa maji, ilikuwa huko—huko chini Meksiko kabla ya ile gharika. Mliliona? Lilikuwa kwenye gazeti, ambako mfumo wa kisasa wa ugavi wa maji kama tu tulio nao sasa, uliozama chini sana ardhini; kitu fulani cha atomiki kikaufunika wote. Ulilipuliwa tu na kufunikwa namna hiyo. Mnaona?

60 Sasa, "kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu," watu werevu, watu werevu wakiwa na nguvu zao za atomiki na kila kitu, wangejenga piramidi na sfiniksi na kadhalika. "Kama ilivyokuwa katika siku hiyo, ndivyo itakavyokuwa." Bali kazi itafupishwa katika siku hii, maana kunapaswa kuwako na watu watakaotwaliwa katika Unyakuo. Kama vile Henoko, kutakuwako na watu watakaovushwa. Tuko kwenye tabaka hilo asubuhi ya leo, watu watakaovushwa kama Nuhu alivyopitishwa kwenye gharika.

61 Lakini kumbukeni, kabla . . . Msisahau hili! Kabla tone moja la mvua kuanguka, kabla hapajakuwapo na kitu kimoja angani, kabla Nuhu haja—hajaikamilisha ile safina, Henoko alipelekwa Nyumbani. Henoko alinyakuliwa pasipo na mauti, alianza tu kutembea siku moja, na—na nguvu za uvutano hazingemzuilia. Ndipo akaona mguu mmoja umeinuliwa juu kidogo, na huo mguu mwingine juu kidogo, na mguu mwingine juu kidogo, na muda si muda mwajua, yeye akasema, "Kwaheri, ulimwengu." Akatembea tu akaingia Utukufuni.

62 Ndipo Nuhu alipoangalia kote asiweze kumwona Henoko mahali popote, aliangalia kote wala hakujua mahali Henoko alipokwenda, ndipo akasema, "Ni wakati wa kuanza kujenga safina sasa." Mnaona? Naye akaanza kuijenga safina ya kuwavusha waliosalia.

63 Hilo ndilo jambo lile lile linalotukia papa hapa. Kanisa lilipelekwa juu Mbinguni, naye Yohana sasa analetwa pamoja Nalo kama mfano wa waliofufuliwa, kama tulivyolichukua jana usiku. Nasi tunaona ya kwamba Sauti ii hii iliyomwita aiangalie dunia tena, ndiyo Sauti ile ile iliyomwita apande juu.

64 Loo, kila Mkristo! Sauti ile ile, Charlie, iliyokuita siku moja huko chini Kentucky, kwamba "Geuka," ndiyo Sauti ile ile itakayokuita, "Panda huku juu!" Hivi huna furaha kwa sababu ya jambo hilo, Ndugu Evans? Sauti iliyosema, "Geuka," Sauti hiyo hiyo ilisema, "Panda huku juu!" Loo, jamani! Hapo, ni miito ya jinsi gani! Ni uhalisi wa jinsi gani! Dhahiri, wazi kama

baragumu, "Geuka, nitumikie Mimi! Njoo huku juu mahali nilipo."

65 Hapo tulimwona akiwakilisha wale waliokufa, Musa kuwakilisha watakatifu waliokufa; wakafufuka. Eliya, pamoja na kundi lake katika siku ya mwisho, pamoja na kundi lake Lililonyakuliwa limesimama pale. Wote mbele ya Bwana Yesu! Yohana alifunua kwamba. . . Yesu aliwaambia ya kwamba a—asingekufa, na iliwapasaje kama akiishi hata akuone kuja Kwake. Nao wanafunzi wakaeneza uvumi.

66 Loo, laiti ningaliingia kwenye kilindi sana, sana sasa hivi, kwa dakika chache, kwa kanisa. Kila mtu anajua. . . Na kila mmoja huishi ma—maisha ya kibinafsi pamoja na Mungu. Ni jambo la kibinafsi, mambo ya Roho yanayokupeleka mahali usingethubutu hata kupazungumzia.

67 Nimeona jambo hili katika maskini huduma yangu ndogo, nyenyekevu, ya kwamba kuna mara nyingi ambapo nitasema jambo fulani na nisijue ni kwa nini nililisema, wala halionekani sawa (Lakini hata hivyo, mtu fulani atasema jambo fulani.), lakini nitaangalia na jambo hilo litatukia kikamilifu tu mahali hapo liwezavyo kuwa. Mungu atalifanya litukie! Ninapotaka tu kusema jambo fulani, nitasema, "Vema, sasa, ngojeni kidogo. Yule *jamaa*, *fulani-wa-fulani*, *hili* litatukia hapa, sasa hilo—hilo halina budi tu kuwa hivyo." Vema, kweli, si—sijui ni kwa nini nililisema. Na muda si muda wajua, ni hivyo tu. Mungu hulifanya!

68 Sasa, wakati wanafunzi hawa walipokuwa wamesema, "Loo, Yesu alisema 'mtu huyu hatakufa.'" Yesu hakusema hivyo kamwe.

Yesu alisema, "Imewapasaje kama akiishi hata nitakapokuja?"

69 Lakini kuwaona wanafunzi wakieneza uvumi wake, basi Yesu alinyosha mkono akamshika Yohana na kumpandisha juu na kumfanya alirudie jambo hilo lote, ayaone mazoezi ya kule Kuja kwa Bwana. Yohana aliliona Kanisa, aliuona mwisho wa wakati wa Kanisa, aliuona mwisho wa Wayahudi, alikuona kule Kuja kwa Pili, aliuona utaratibu wote.

70 Basi angalieni kile kilichompasa Mungu kufanya; kumchemsha kwenye grisi kwa muda wa yapata saa ishirini na nne kule chini, kuwafanya waone kwamba yeye alikuwa ni wa Kiungu, ya kwamba Roho wa Kiungu alikuwa amemtia mafuta ki—kinafsi. . . (hiyo ni nje, ya udongo, ama vyovyote mnavyouita, mwili wa mwanadamu), alikuwa amemwingia Kiungu sana hata grisi yenye joto iliyochemshwa saa ishirini na nne hata haikumwunguza. Wakijaribu kumchemsha Roho Mtakatifu amtoke mtu; huwezi kufanya hivyo. Wakamweka huko nje kwenye kisiwa cha Patimo, naye akaandika Kitabu, kisha akarudi na kuhubiri miaka kadhaa. Hmm. Hmm.

71 Hakika, sasa, ilimbidi kuchukua jina baya, "Alikuwa mpiga ramli, alikuwa ni mchawi." Ni wangapi wanaojua kwamba Yohana aliitwa mchawi? Kweli kabisa! Yesu aliitwa hivyo, pia. Mnaona? Mnaona, ulimwengu haujui lolote kuhusu mambo haya. "Alikuwa msoma mawazo." Mnaona? Walisema kwamba "Alikuwa mchawi hodari sana hata akairoga grisi hiyo, hata hiyo grisi isingeweza kumchoma kwa sababu alikuwa ameiroga," kwa sababu tu hakukubaliana na mawazo yao ya Kikatoliki. Hivyo tu.

72 Yeye alikuwa mtumishi wa Mungu ambaye . . . mnyenyekevu, alikuwa na misheni ndogo huko chini aliyoidumisha. Asingeyavumilia mambo hayo makuu ya kale, na kwa hiyo Mungu alimlinda tu na kumhifadhi. Vivyo hivyo aliwahifadhi: Mtakatifu Martin na—na Ireneo, na wote kote katika wakati.

73 Naye anafanya jambo lile lile leo hii, anashuka moja kwa moja. Sasa, kamwe msisahau hili, ya kwamba Mungu aliahidi mitikiso mikubwa, na kazi kubwa, kubwa mno. Sasa, andikeni hili katika muhtasari wenu mnaoandika (Mnaona. Mnaona?), kwamba kile mwanadamu anachoita "kikuu na chenye nguvu," Mungu hukiita "Upumbavu!" Na kile mwanadamu anachoita "upumbavu," Mungu hukiita "Kikuu!" Msisahau hilo, mnaona, msilisahau. Hilo litawasaidia katika miaka ijayo, kwa kuwa tunatazamia jambo kuu zaidi wakati wote. Nasi tunapokea lililo kuu zaidi wakati wote, bali walimwengu hawajui. Wala hawakujua katika siku za Nuhu, wala hawakujua katika siku za Yohana, katika siku za Yesu, katika siku za mitume, katika siku za Ireneo, yoyote ya siku hizo, hawakujua.

74 Hata Joan wa Arc, yeye alikuwa ni maskini mwanamke mtakatifu. Wakati hakuwa kitu ila msichana, Mungu alisema naye katika maono, na Malaika akasema naye. Mnajua kile kanisa Katoliki lilichosema? "Yeye ni mchawi." Nao wakamweka kwenye nguzo na kumchoma moto akafa, makasisi wa Katoliki walifanya hivyo; walimwua, wakamhukumia kifo kama "mchawi," naye Joan wa Arc akafa kama mchawi. Yapata miaka mia mbili baadaye, wakakuta kwamba hakuwa mchawi, alikuwa m—mwanafunzi wa Kristo.

75 Walifanya jambo lilo hilo kwa watakatifu wote. Yesu alisema, "Ni yupi kati yenu baba zenu hawakumtesa? Ni yupi kati ya manabii waliopata kuja ambaye hawakumkataa?" Kasema, "Enyi kuta zilizopakwa chokaa." Kasema, "Mna—mnashuka na—na kupaka chokaa juu ya makaburi ya manabii, nanyi ndio hasa mliowaweka mle ndani." Hmm! Jamani! Jamani! Mnaona? Hakuwachezea kamwe. Hmm! Aliwaambia tu.

76 "Kizazi hiki cha nyoka," Yohana alisema, "ni nani aliyewaonya kuikimbia ghadhabu ijayo? Msianze kusema mna

Ibrahimu baba yenu." "Sisi ni wafuasi wa madhehebu fulani, makubwa."

"Wewe ni Mkristo?"

77 "Loo, Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mpentekoste." Hilo haliko ndani yake hata kidogo. Hilo halina uhusiano wowote nalo kuliko—kuliko—kuliko—kuliko—kuliko theluji ilivyo na nuru ya jua. Mnaona? Halina uhusiano wowote nalo. Kama wewe ni Mkristo, wewe ni mtumishi wa Mungu aliyezaliwa mara ya pili.

78 Sasa, sasa, wakati Yohana alipokuja, tulikuwa nalo jana usiku. Sasa, kumbukeni, mnapofikia kwenye hili . . . Kwa ajili ya muktadha wa jambo hilo, ni—niliwaambia basi. Kumbukeni, ulimwengu unapata mtikiso wenye nguvu sana uliopata kuwa nao, sasa hivi, ulimwengu wa kanisa.

79 Sasa, kumbukeni, hapana shaka, katika siku za—za Yohana, siku za Yesu, kulikuwako na sherehe kuu na wasemaji hodari katika siku zao, watu wakuu wenye akili, nao wakawavuta makumi elfu mara maelfu ya watu. Kayafa angefanya nini kama angaliitisha m—mkutano pamoja? Angeileta Yerusalemu nzima, angewaleta Israeli wote pamoja, kutoka kila pembe. Na wote waseme, "Loo,"

"Sasa, kama Kayafa anasema mambo *fulani-fulani*, hilo litakuwa ni zuri sana."

"Loo, je, unaamini Maandiko, Rabi, Kasisi, Daktari, Askofu? Unaamini Maandiko?"

"Hakika, ninayaamini Maandiko, mimi ni mwanachuoni mashuhuri!"

80 "Vema. Sasa, Biblia ilisema hapa ya kwamba utakuja wakati ambapo kutakuwako, 'Milima yote itaruka kama wana-kondoo wa kiume, majani yote yatapiga makofi yao, na mahali pote palipoinuka patashushwa na kufanywa bonde, mabonde yote yatainuliwa na kukuzwa. Na yatafanywa na sauti ya mtu aliaye nyikani.' Unaamini hilo, Rabi, Kasisi, Daktari, Mchungaji?"

"Hakika, ninaamini hilo!"

"Itafanyikaje?"

81 "Loo, Mungu atamtuma mtu mwenye nguvu duniani siku moja. Loo, atakuwa mkuu. Atakuwa sauti ya mtu aliaye nyikani, ama atamtangulia Masihi ajaye. Basi ajapo, hapana shaka niani mwangu ila kwamba atashuka kutoka Mbinguni na kuja hekaluni. Atashuka moja kwa moja hapa hekaluni, na kusema, 'Sasa, tutawachukua Warumi wote na kuwapiga hata wafe. Hivyo tu. Tutawapiga Warumi wote.' Na—na kisha atasema, 'Shuka chini, ewe Masihi!' Naye Masihi atashuka, nasi tutafinyanga miundu yetu yote ya kupogolea iwe . . . ama panga zetu ziwe majembe ya kulima na miundu ya kupogolea, wala hakutakuwako na vita tena." Na, a-ha, hiyo ndiyo fasiri yao.

82 Lakini ilikuwaje wakati lilipotukia? Kulifanyika nini? Hapakukuwako na maonyesho ya Mbinguni, yale waliyopata kuona; kulikuwako na moja, bali hawakuliona. Hawakuliona. Mnaona. Ni wakati gani milima yote iliporukaruka kama wanakondoo wa kiume? Ni wakati gani mahali pote palipoinuka paliposhushwa nayo mabonde yakainuliwa? Maskini mhubiri mwenye nywele za kitimtimu alikuja akitembea kutoka nyikani wala hata hakujua ABC zake. Kulingana na historia, alienda nyikani akiwa na umri wa miaka tisa wala hakuonekana tena mpaka kwenye umri wa miaka thelathini. Alikula nzige na asali mwitu. Nzige ni panzi, wale panzi warefu.

83 Wanawala wakati wote. Vema, unaweza kuwanunua papa hapa kwenye. . .Sidhani hao ni wabaya, maana unaweza kuwanunua papa hapa kwenye supamaketi ukiwataka, nyukimanyoya, nyukiasali, nzige, nyoka mchacharika, chochote unachotaka, unaona.

84 Kwa hiyo aliishi kwa nzige na asali mwitu. Mlo wa jinsi gani! Bali alidumishwa na nguvu za Mungu. Yeye hakuvaa ukosi uliopinduliwa; kama vile mtu fulani alivyosema jana usiku, Ndugu Parnell ama baadhi yao. Hakuvaa koti rasmi lenye mkia, na yote kuhusu hayo. Alitoka nyikani amejizungushia kipande kikubwa kichakavu cha ngozi ya kondoo. Kama vile nimesema, labda . . .Inatubidi kuoga kila siku, na labda hakuoga siku moja kwa kila miezi mitatu ama minne, huko nje nyikani. Sijui. Hakuonekana wa kupendeza sana. Hakuwa na mimbara yoyote. Hakuingia kwenye miji mikubwa yoyote na kufanya miamsho mikubwa. Alisimama huko nje ukingoni mwa Yordani, matope yamefikia magotini mwake, na kusema, "Enyi uzao wa nyoka, ni nani aliyewaonya kuikimbia ghadhabu ijayo?" Hmm. Hapo ndipo mahali palipoinuka paliposhushwa, mnaona, na mahali palipo chini kuinuliwa. A-ha. Naam, bwana.

85 Halafu, muda si muda wajua, walikuwa wakimtarajia Masihi kushuka pamoja na Malaika na kadhalika, na kuketi kwenye kanopi huko nje na hekaluni ambapo walikuwa wamemjengea Yeye apate kujia (kama vile tunavyojenga sehemu kubwa kubwa leo hii kote katika mataifa na kadhalika). Mnaona? Naye alikuja lini? Alipita kila moja ya hayo masinagogi, kila moja ya hayo madhehebu, na kushuka kwenye zizi. Walimlazimisha kuingia ndani yake.

86 Hivyo ndivyo ilivyo leo. Analazimishwa kuingia katika vitu, analazimishwa kufanya hivyo, analazimishwa kuwa asiyefungwa na madhehebu, kwa sababu Ujumbe Wake haushirikiani na dhehebu. Ujumbe Wake leo hii, unaohubiriwa na wahudumu Wake, ni usiofungwa na madhehebu maana madhehebu yalimtupa nje. Biblia ilisema hivyo. Alikuwa nje, akibisha, akijaribu kuingia (Mnaona?), katika kanisa Lake Mwenyewe. Hapo ndipo ulipo. Mnaona, ni vile vile leo hii.

87 Kwa hiyo, kumbukeni, kinachoonekana kikubwa kwa mwanadamu, ni kidogo mbele za Mungu. Sasa, hiyo ndiyo sababu haikubidi kuwa na maua mengi sana. Ndipo wakati Mungu atakapokuja tena, wakati Yesu atakapokuja tena, utashangaa, maskini yule mwanamke mfua nguo kichochoroni. Uh-hum. Utashangaa, huyo jamaa ambaye hasemi chochote, anayejiwekea siri zake mwenyewe na kutembea huku na huku mbele za Mungu, mnyenyekevu. Utashangaa. Itakusha-. . .

88 Nilihubiri si muda mrefu uliopita, kwenye hukumu. . . *Mishangao Hukumuni*. Haitashangaza kumwona mwuza pombe haramu kule, anajua anaenda. Hakika. Haitashangaza kumwona mwongo, mzinzi, kila kitu kule, hao sio. Ila mshangao utakuwa, na sikitiko litakuwa, wale wanaofikiri wanaenda; a-ha, naam, kisha wakataliwe. Wale waliosema, "Vema, ngoja kidogo, mama yangu alikuwa mfuasi wa kanisa hili, baba yangu alikuwa mfuasi wa kanisa hili, babu yangu na nyanya yangu. Nimekuwa mfuasi kule maishani mwangu mwote."

89 "Ondoka Kwangu, ewe mtenda maovu, hata sikukujua."

90 Angalieni kwenye siku ambazo maskini mzee Simeoni, mtu asiyejulikana, hana sifa, hatujui lolote kumhusu katika Biblia. Lakini Biblia ilisema, "Ilifunuliwa kwake na Roho Mtakatifu," (Huyo hapo; haya basi.) "kwamba asingekufa hata atakapomwona Kristo wa—wa Bwana."

91 Basi angalieni Yohana Mbatizaji alikuwa ni nani, namna fulani ya mtu wa kipekee, mtu wa mwituni huko nje mwituni. Ilifunuliwa kwake. Alitokea akihubiri Ujumbe. Angalieni hilo!

Maskini Ana alikuwa ni nani?

92 Maskini yule bikira, Mariamu, huko chini ka—katika mji wa Nazareti (mbaya kama Jeffersonville) na ambako kulijaa dhambi na kila kitu, bali alikuwa amejiweka safi kwa kuwa alijua siku moja atakuja Masihi. Mnaona?

93 Yusufu, seremala, alikuwa amempoteza mke wake na—naye alikuwa akimchumbia maskini msichana huyu. Na ilikuwa ni kupitia hapo ambapo Roho Mtakatifu alimjia huyo. Ndipo walimwengu wanakuja huku na kumpa jina baya, kama vile "mtakatifu anayejibingirisha, mpentekoste." Mnaona, wakampa jina baya. "Mbona, hilo, yeye. . .mtoto huyo alizaliwa nje ya ndoa takatifu." Mnaona, waliamini hilo, na ilionekana kama ndivyo ilivyokuwa. Lakini Mungu hufanya hivyo kuyapofusha macho ya wenye hekima na elimu, na kuwafunulia watoto wachanga watakaojifunza.

94 Ninatumaini kuna msingi wa kutosha nitakapofikia jambo fulani baada ya kitambo kidogo. Nitawaonyesha. Mnayaona mafuta haya? Sasa, kile nimewaambia, msingi, kuona ya kwamba sio mwanadamu, ni Mungu, nitaelekeza kwenye *hiki*. Vema.

95 Sasa, “Njoo huku juu,” ilikuwa ndiyo Sauti. Na wakati alipofungua alisikia sauti ya parapanda, ndipo mara moja Yohana alikuwa katika Roho—alikuwa katika Roho, na mara alipoingia katika Roho alianza kuona mambo. Unaanza kuona mambo unapoingia katika Roho. Kwanza lazima uingie katika Roho. Hiyo ni kweli?

96 Sasa, vipi kama ulienda kwenye mchezo wa mpira, nawe ukasema, “Hakika ninaipenda besiboli.” Um-hum. Nawe ujipatie kiti cha safu ya mbele, moja kwa moja kwenye kiti cha mbele nawe unawaangalia Wayankii ama Bulldogs, wowote wale, wakicheza. Nao wote wana mchezo moto-moto huko nje.

97 Nao upande wako uko karibu kushindwa, na mara Mtoto Ruthu mamboleo anazungusha gongo lake namna *hii* na kusema, “Mnaona kule?” Ana watu watatu kituoni. “Whaap!” Naye anaurusha mbali usionekane tena; anatoa kofia yake na kujipepea; anashuka kwenye kituo cha kwanza na kuangalia kote, hao jamaa wote; anaenda kwenye kituo cha pili, anampa mkono mtu wa kituo cha pili; anaenda, anarudi kimya moja kwa moja nyumbani, anainamisha ninii yake . . . Mbona, jamani! Jamani! Mayowe, kurukaruka, vifijo, makelele ya “Huree!” Mbona, wangeninii . . .

98 Kwa kweli nimewaona wakichukua hizi . . . Mnakumbuka ile kofia ya kale ya nyasi? Nilienda kwenye mchezo wa besiboli siku moja na kuona jamaa akiingiza goli. Naye huyu jamaa aliyeketi mbele yangu amevaa kofia ya nyasi, alishikwa na msisimko sana; akashika kofia yake na kuivuta chini kabisa, akajifungia ukosi namna *hii* ambapo sehemu ya juu ilitoka. Mbona, alikuwa na wakati mzuri sana! A—alikuwa hajitambui kabisa hata hakujua alichokuwa akifanya. Kurusha mateke tu na kushangilia na kupiga makelele na kurukaruka. Vema, sasa, mnajua ninalowazia, hakika alikuwa na . . . alikuwa ninii . . . alikuwa . . . aliipenda besiboli. Alikuwa shabiki wa besiboli, kama tu vile shabiki wa sigara ama shabiki wa wiski.

99 Mimi ni shabiki wa Yesu. Naam. Ninapenda tu hilo. Mimi . . . Ukipata kuwa shabiki wa Yesu, unaona, shabiki wa kitu fulani.

100 Basi ungeweza kumwazia jamaa huyo akisema, “Loo, hakika, mimi ni shabiki wa besiboli.” Na upande wake uko karibu kushindwa, nao wamwone akitokea na kushinda mechi jinsi hiyo, aliangalia kote kisha, “Naam, nadhani huo ulikuwa ni sawa.” Uh-huh. Aseme, yeye “anaipenda besiboli.”

“Loo, yeye ni kitu fulani!”

101 Ungesema, “Mbona, huipendi, sivyo? Una kasoro!” Kila shabiki mzuri wa besiboli angesema, “Kwani yule jamaa ana shida gani? Ana kasoro. Mwangalie akiketi pale.” Haah! Hilo ni ninii sana . . .

102 Weka mbili na mbili pamoja sasa, unaona. Loo, unapokuwa shabiki wa Yesu, nawe unamhisi Roho Mtakatifu akizama

kwenye Maneno hayo, basi kitu fulani kinapaza sauti! Loo, unajisahau!

103 Natumaini mtu huyu atanisamehe, ameketi hapa karibu. Jamaa huyu mkubwa, mrefu, mwenye nywele nyeusi anayeketi hapa, aliyekuwa amesimama huko nje sebuleni, ndipo mtu fulani akasema jambo fulani la. . .usaidizi, mwajua, kwa namna fulani akambariki namna hiyo. Na maskini mvulana huyu amekuwa na wakati mbaya sana, najua mke wa—wake alimwacha na kumshtakia talaka kwa kuwa alimpenda Bwana Yesu. Hiyo ni kweli. Ndipo mtu fulani akasema jambo fulani kumhusu Yesu, mwajua, kidogo alikuwa ni mmoja wa hao mashabiki. Naye alikuwa vitani na akapigwa risasi kila mahali, na kila kitu, huyo mvulana alikuwa; nilimhurumia. Alikuja nyumbani na. . .watoto wake na mkewe. Ndipo a—akamwahidi Bwana angemtumikia, na mara Bwana alipoanza kumbariki na akajiweka sawa na Mungu, mke wake alimgeuka tu, akamshtakia talaka na kumwacha. Akamwacha peke yake. Bali angali alikuwa ni shabiki.

104 Basi wakati aliposimama pale usiku mmoja na mtu fulani akasema jambo fulani kumhusu Yesu, jambo fulani, jinsi alivyokuwa ni mkuu, namna hiyo, yeye alisema, "Loo, Utukufu!" Akairusha mikono yake nayo ngumi yake ilikuwa imetokeza ukutani namna hiyo. Hakujua alikuwa amefanya hivyo. Ngumi yake ilikuwa imetokeza ukutani. Kasema, "Ndugu Bill, nitalipia hilo." Nafikiri Ndugu Wood alikuja na kuutia kiraka, akabandika kipande kingine. Hatukujali hilo, Ndugu Ben, tulininii tu—tulikuwa na furaha ulikuwa shabiki. Mnaona?

105 Roho Mtakatifu anapokufanyia jambo fulani, kamwe huwezi kuketi kimya, kuna kitu fulani kinachobubujika. Amina. Whiu! Naam, kitu fulani kinashikilia, shabiki wa Kristo. Unapompenda Bwana, kitu fulani tu ndani yako kikinyosha mkono, kikishika kwa nguvu, kikiona njaa na kiu, Yesu alisema, "Heri wao, kwa maana watajazwa. Heri wao hata kuona kiu, kama unacho ama huna." Ni wangapi wanataka Mungu zaidi? Vema. Vema, sababu ya wewe kutaka zaidi ya Mungu, umebarikiwa kuwa tu hivyo. Kama huna, ungali umebarikiwa. "Na heri ni wale walio na njaa na kiu." Umebarikiwa kuona tu njaa na kiu. Kwa kuwa unamtaka, umebarikiwa. Kwa sababu kuna watu wengi ambao hawamtaki.

106 Mnakumbuka somo langu hivi majuzi usiku? Mnaona, kama vile yule punguani, aliweka kibweta nayo zawadi akaitupilia mbali. Mnaona? Usikichukue kibweta, chukua Zawadi. Vema.

> Sasa *mara. . .katika roho: na tazama, kiti cha enzi. . . kimewekwa mbinguni na mmoja ameketi* juu ya *kile kiti.*

107 Sasa, angalieni, baadaye kidogo, ama, tulilipata jana usiku, ninaamini, ya kwamba juu ya Kiti hiki cha Enzi ambacho. . .

Tunaona ya kwamba kwanza hapakuwapo na kitu chochote juu ya hicho Kiti cha Enzi, na sasa kuna Mtu fulani juu ya hicho Kiti cha Enzi kwa hiyo ilionyesha ya kwamba Yesu alikuwa amekuja pamoja na Kanisa Lake Utukufuni na alikuwa ameketi kwenye Kiti Chake Mwenyewe cha Enzi. "Ameketi kwenye Kiti cha Enzi," hiyo ni baada ya wakati wa Kanisa. Sasa, sasa, tunataka kufikia hilo baada ya kitambo kidogo.

108 Sasa, unasema, "Vema, kiti Chake cha enzi kiko wapi leo?" Sasa, Ndugu Neville, kama nikipita hilo, niulize baada ya kitambo kidogo, "Kiti Chake cha enzi kiko wapi siku hizi." Nafikiri nitakifikia umbali huo. "Kiti Chake cha enzi kiko wapi sasa ikiwa Yeye hayuko kwenye Kiti Chake cha Enzi sasa?"

Yeye hayuko kwenye Kiti Chake cha Enzi sasa. La, bwana.

109 Vema, sasa:

> *Na yeye aliyeketi alionekana mithili ya. . .jiwe la yaspi na. . .akiki, na upinde wa mvua* ulikizunguka *kile kiti cha enzi,* ukifanana. . .*ukionekana mithili ya zumaridi.*

110 Sasa, hebu tuchukue sasa kifungu cha 3, kuanza. Na kwa hiyo "yaspi," Huyu aliyeketi kwenye Kiti cha Enzi alionekana. . .Kwa maneno mengine, ulipomwangalia, Yeye alikuwa katika fahari kuu sana, uzuri! Loo, ninataka kumwona. Nawe je?

111 Siku moja. . .Ninamkumbuka Dada Cadle, Dada Howard Cadle, nafikiri wengi wenu mnamkumbuka. Nilikuwa upande wa pili wa barabara pale, na mke wangu anayeketi pale sasa anakumbuka alikuwa baridi, chumbani. Nami nilikuwa nimeamka, na nilikuwa na maskini ninii. . .lilikuwa ni jiko la tumbili huko nje pamoja na. . .tulioka mikate yetu kwenye jiko, katika bomba. Na mimi. . .ilikuwa baridi sana na upepo ulikuwa ukivuma, wakati wa baridi kali, theluji ardhini, na upepo ukishuka kwenye dohani, wala nisingekifanya kitu hicho kuwaka, kuyaokoa maisha yangu. Nami nilikuwa nimechanganyikiwa kabisa kukihusu. Ndipo nikaingiza baadhi yake, nacho kingezima tena. Billy alikuwa baridi na mamaye baridi, nilikuwa nikijaribu kuwasha moto. Ndipo ikatokea nilifungulia redio na (dakika chache hapo awali, ndipo tu ikawa joto, ikaja), naye Dada Cadle alikuwa akiimba, "Nitakapofika kwenye Nchi hiyo, kwenye pwani ya mbali, ninataka kumwona Yesu. Nawe je?" Loo, jamani!

112 Niliketi tu papo hapo chini katikati ya sakafu na kuketi tu hapo na kuanza kulia. Mnajua jinsi angeweza kuimba, chini, kutoka kwenye hiyo sauti yake tamu ya ndege mwigo. Ninataka kumsikia nitakapovuka mpaka huko ng'ambo; kasema, "Ninataka kumwona Yesu. Nawe je?"

113 Nikawazia, "Ee Mungu, naam, ninataka kumwona siku moja. Wakati maua yote yatakapopita, ninataka kumwona

Yesu." Jinsi...Kumwona juu ya Kiti Chake cha Enzi, uzuri Wake, fahari Yake! Na kama mimi...Loo, ninataka kusimama ambapo Yohana alisimama, kusudi niweze tu kusimama na kumwangalia.

114 Hapa wakati fulani uliopita, chini... ule wakati wa utumwa. Ninasema hili kwa niaba ya marafiki wangu weusi walio hapa asubuhi ya leo. Kulikuwako na maskini mtu mweusi, naye alikuwa...alikuwa akienda mahali padogo, walipozoea kwenda.

115 Nao walikuwa wakifanya hili huko Kentucky, kuimba. Labda Mama Cox na hao wengine wanaweza kukumbuka wakati walikuwa wakienda na kuimba, mwajua, kwenda kwenye nyumba na kucheza kinanda, vijana na hao wote wanaimba. Walikuwa wakifanya hivyo hapa juu Utica, na mahali pote barani. Sasa wana kisaga cha wiski, huko nje mahali fulani kwenye karamu ya roki.

116 Lakini, wakati huo, waliimba nyimbo za dini. Mmoja wa huku kuimba nyimbo za kale za dini, kulikuwako na ndugu mzee mweusi, aliyeokoka. Ndipo Bwana akamwita kuhubiri, basi kesho yake alienda kote akiwaambia watumwa shambani. Akasema, "Bwana aliniokoa jana usiku na ameniita kuwahubiria ndugu zangu."

117 Basi hatimaye ikamfikia mwenye ranchi ama mwenye shamba. Akamwita ndani, kasema, "Sambo, ninakutaka, ingia hapa." Kasema, "Panda uje ofisini mwangu."

Akasema, "Naam, bwana," akaenda ofisini.

118 Akasema, "Ni kitu gani hiki ninachosikia unasambaza miongoni mwa watumwa, miongoni mwa hao jamaa huko nje, wafanyakazi wangu, watumwa wangu, ya kwamba Bwana alikuweka huru?"

119 Kasema, "Naam, bwana." Akasema, "Bosi, mimi ni mtumwa wako." Akasema, "Nilinunuliwa na fedha zako, lakini..." Akasema, "Bali jinsi Bwana alivyonifanya huru jana usiku, Yesu alinifanya huru na maisha ya dhambi na aibu, na maisha ya mauti. Aliniweka huru."

Akasema, "Sambo, kweli unamaanisha hilo?"

Akasema, "Ninalimaanisha."

120 Akasema, "Niliwasikia wakisema utaanza kuhubiri huku kwa ndugu za—zako shambani na kadhalika."

121 Kasema, "Naam, bwana!" Kasema, "Hivyo ndivyo ninavyokusudia kufanya, ni kuihubiri Injili hii kwa ndugu zangu."

Kasema, "Kweli unamaanisha hilo, Sambo?"

Akasema, "Kweli ninamaanisha."

122 Kasema, "Njoo, twende pamoja ma—mahakamani, pia nitakupa uhuru wako. Uko huru nami, nawe u huru na utumwa zaidi. Nilikununua, wewe ni wangu, nami ninakuweka huru ili uweze kuihubiri Injili kwa ndugu zako." Akashuka akaenda na kutia sahihi ukombozi, ama tangazo, naye akawekwa huru. Asingeweza tena kuuzwa kama mtumwa. Alikuwa mtu huru kuihubiri Injili.

123 Alihubiri miongoni mwa nduguze kwa miaka kadhaa. Wazungu wengi waliongoka chini ya huduma yake. Siku moja mzee huyo alifikia kifo chake. Alikuwa amehubiri kwa muda wa miaka thelathini ama arobaini, ama zaidi. Ndipo alipofikia kifo chake, alikuwa amelala chumbani, na wengi wa ndugu zake wazungu walikuwa wamekusanyika chumbani nao wakafikiri alikuwa amewaacha kwa karibu saa mbili ama tatu. Ndipo wakati hatimaye alipoamka na kuangalia huku na huku chumbani, alisema . . .

"Ulikuwa wapi, Sambo?"

Akasema, "Loo, ni mimi nimerudi hapa tena? Kwani ni mimi nimerudi tena?"

Wakasema, "Kuna nini, Sambo?"

Kasema, "Loo, nilivuka nikaingia Nchi ile nyingine."

Wakasema, "Hebu twambie kuihusu."

124 Akasema, "Vema, ndiyo kwanza niingie, katika Uwepo Wake." Kisha kasema, "Niliposimama pale," akasema, "huyu hapa Malaika anaingia, kasema, 'Jina lako ni Sambo *Nanii wa nanii*?'"

Akasema, "Naam, bwana, ndivyo."

Akasema, "Karibu."

"Nikaingia ndani, nami nikamwangalia ameketi pale."

125 Akasema, "Sambo, njoo hapa sasa, ukiisha kumwona Yeye ninakutaka, uje hapa nje, tunataka kukupa vazi lako, tunataka kukupa kinubi chako, tunataka kukupa taji yako."

Sambo akasema, "Msiniambie juu ya vinubi, taji, na mavazi."

Kasema, "Lakini umeshinda thawabu, tunataka kukupa thawabu yako."

126 Kasema, "Usinizungumzie . . . kunihusu mimi . . . kuhusu tuzo." Kasema, "Niache tu nisimame na kumwangalia Yeye kwa muda wa miaka elfu moja. Hiyo itakuwa ndiyo thawabu yangu."

127 Nafikiri hivyo ni kama vile sisi sote tungejisikia, "Niache tu nisimame na kumwangalia Yeye." Loo, itanibidi kuwa na mwili tofauti na nilio nao sasa, kila unyuzi wa utu wako kumwangalia tu.

128 Hapo Yohana alisimama na kumwona Yeye ameketi kwenye Kiti cha Enzi, Naye "alionekana mithili ya jiwe la yaspi na akiki." Sasa, mambo yote na kila neno lina maana katika Biblia. Sasa, "jiwe la yaspi na akiki."

129 Sasa, kama mtaona, inalingana na Maandiko mengine. Katika sehemu za nyuma ya Maandiko, Yeye alikuwa Alfa, Omega, alikuwa ni Mwanzo na Mwisho, alikuwa wa Kwanza na wa Mwisho, alikuwa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Alikuwa "yote kwa yote" imelundikwa ndani Yake. Mathayo 17 inaonyesha ya kwamba Yeye...huko kwenye Mlima wa Kugeuka sura, yote yalikusanyika katika Yeye.

130 Sasa, "yaspi" lilikuwa—lilikuwa ni jiwe, na "akiki" lilikuwa ni jiwe. (Sasa, tutaziendea rangi zao baada ya kitambo kidogo.) Sasa, ninawatakeni muone ya kwamba kila mmoja wa wale wazee wakati walipozaliwa, naam, kila mtu, ana jiwe la uzawa. Langu, nilizaliwa Aprili, almasi. Na miezi mbalimbali inawakilisha mawe mbalimbali. Vema, wale wazee walikuwa vivyo hivyo. Kila wakati ambapo mzee, wakati alipozaliwa, aliku-...alikuwa na jiwe la uzawa.

131 Na kusimama tu papa hapa kwa muda kidogo tu. Wakati hao mama wa Kiebrania...Hebu nikuonyeshe Neno la Kiungu, rafiki, kusudi imani yako ijengwe imara katika Neno la Mungu. Kila wakati, hao mama wa Kiebrania, walipokuwa katika utungu wa kuzaa, wakiwa na utungu wa kuzaa, kujifungua... kuwazaa watoto hawa, maneno yenyewe ambayo alitamka katika kuzaa kwake yalimpa mtu huyo (mtoto huyo mchanga aliyemzaa) jina lake, na kumweka mahali pake katika Palestina ambako atakuwa katika kule kuja kwa Bwana. Utungu wa kuzaa wa mama huyu! Kama vile, *Efraimu* maana yake ni "karibu na bahari." Mnaona? Naye Efraimu alipewa sehemu yake karibu na bahari. Na, tuseme, *Yuda* lilimaanisha...sijui neno hilo linamaanisha nini, bali ningeweza kulipata. Sasa, mnaona, hapo ndipo sina wakati, mambo haya mafupi, kuyachukua mambo hayo. Lakini basi rudini nyuma, na *Yuda,* popote Yuda linapomaanisha, ilimaanisha mahali pake alipowekwa miongoni mwa wana wa Israeli.

132 Na mkichukua Mwanzo 48 na 49, mtaona huko kwamba Yakobo, wakati alipokuwa akifa, akiegemea kwenye fimbo yake, kipofu, yeye aliwaelezea hao watoto mahali watakapokuwa mwishoni mwa ulimwengu. Nao wamekaa mahali papo hapo sasa kwa kuwa wamerudi kwenye nchi ya uenyeji wao. Akamwambia Yusufu, "Wewe ni mzabibu uzaao karibu na ukuta," unaona, "karibu na kisima," maji. Akaenda huko. Akasema, "Umemtumaini Bwana Mungu. Uliimarisha u—upinde wako" (Marekani. Mnaona?) "katika Bwana, bali siku moja mzabibu huo ulikuwa ukirudi juu ya ukuta." Naye huyo hapo, pale pale sasa. Kile hasa alichosema karibu miaka elfu tatu iliyopita, akirudi moja kwa moja. Akamwambia Efraimu

alikuwa ameitumbukiza miguu yake kwenye mafuta, naye Efraimu alikaa pale pale penye vile visima vikubwa vya mafuta. Vivyo hivyo hasa.

133 Matamshi ya watu hao, ni kitu gani kilikuwa kwenye wanadamu hao? Mungu akichukua nyuzi zao na kutenda kazi ndani yao!

134 Ilionekana kana kwamba wakati ile Himaya ya Kirumi ilipowatawanya, wakati hao wengine walipowatawanya, wakati walipochukiwa na Hitler, makumi elfu mara maelfu, aliwadunga matone ya sumu kwenye mishipa yao nao wakafa, ungeweza kuona miili yao ikining'inia kwenye nyua pamoja na watoto wao wachanga na kila kitu kingine, na mifupa . . . kisha akaiokota na kutengeneza mbolea kutoka kwa mifupa yao. Wanawapeleka tu kule nje na kuwadunga sindano, wakawaweka kwenye behewa. Kisha wakatoka, wakati walipotoka, hata mwanzoni, walikuwa wakiimba, "Masihi atakuja nasi tutakunywa damu ya mzabibu tena." Waliposhuka, wakifa, hao Wayahudi, wakitembea moja kwa moja huko nje, wakijua mapigo mengine machache tu zaidi na moyo wao utasimama. Na wangeshuka, wakiimba, "Tutamwona Masihi hivi karibuni." Loo, jamani! Wakitengeneza mbolea kutoka kwa mifupa yao.

135 Wengi wenu askari hapa ndani mnajua hilo na mmeliona. Nilisimama mahali walipowateketeza kwa moto na kila kitu kingine, pale, Hitler na hao wengine. Kisha mwangalie Stalin na Urusi na hao wote, walifanya jambo lile lile. Hiyo ni kweli. Lakini Myahudi huyo, shida ilikuwa ni nini? Alilazimishwa kurudi kwenye nchi ya uenyeji wake. Hapo ndipo wanaposimama.

136 Sasa, ninayo filamu ile mashuhuri, *Dakika Tatu Kabla Ya Usiku wa Manane*. Wakati Wayahudi walipoingia, walikuwa wakiwauliza, kasema, "Kwa nini mnarudi, mpate kufia kwenye nchi ya uenyeji wenu?"

137 Kasema, "Tumekuja kumwona Masihi." Amina. Hmm! Tuko kwenye wakati wa mwisho.

138 Kila mmoja wa watoto hao wakati walipozaliwa, walikuwa na jiwe la uzawa. Na wakati Haruni, yule kuhani mkuu juu ya kila mmoja wa watoto hao, alikuwa amevaa naivera, nguo yake. Hapo ndipo ninapotaka kushikilia kwa muda kidogo zaidi, kufikia kwenye kifungu hiki cha 6, kwa maana hiyo inaingiza kila mfano wa Agano la Kale moja kwa moja mle. Kila . . . fenicha zote na kila kitu katika Agano la Kale ilikuwa ni mfano wa vilivyoonekana Mbinguni, vikafananishwa tena kwa mwanadamu.

139 Na hii hapa naivera ya Haruni, yeye alikuwa ni kuhani mkuu. Angalia, jiwe la uzawa wa kila kabila liliwakilishwa mle ndani. Moja, jiwe la uzawa, akaweka jiwe lake mle ndani; kabila la Efraimu, kabila la Manase, kabila la Gadi, kabila la Benyamini,

wote waliwakilishwa hapa ndani. Na hivyo ndivyo. . .Ndipo wanayachukua mawe hayo ya uzawa, vito hivyo vizuri, na kuvining'iniza kwenye nguzo namna hii. Ndipo kama nabii alitabiri, na kama ulisikika ni wa kweli ama si wa kweli, walimpeleka kwenye Urimu Thumimu hii na kumwacha atoe unabii wake; kama kuna Nuru takatifu iliyotokea pale na kuanza kuyamulika mawe haya pamoja, ilikuwa ni Mungu akijibu. Ilikuwa ni kwa ajili ya kabila lote, wote, kila kabila.

140 Sasa, kwenye haya, jiwe la kwanza. La kwanza, ni wangapi wanaojua mtoto wa kwanza alikuwa ni nani? Jina lake lilikuwa ni nani? Rubeni. Vema. Wa mwisho alikuwa ni nani? Benyamini. Hiyo ni kweli. Jiwe la uzawa la Rubeni lilikuwa ni "yaspi," jiwe la uzawa la Benyamini lilikuwa ni "akiki." Alionekana mithili ya "Rubeni na Benyamini," wa Kwanza na wa Mwisho, Yeye Aliyekuwako, Aliyeko, na Atakayekuja, Yeye alikuwa ni Alfa (A) katika alfabeti za Kiyunani, Omega (Z) katika alfabeti za Kiyunani. Alikuwa ni wa Kwanza, wa Mwisho, alikuwa tangu Benyamini hadi Rubeni, tangu Rubeni hadi Benyamini. Loo, jamani! Huyo hapo, "Alionekana mithili ya jiwe la akiki na jiwe la yaspi." Alikuwa ameketi juu ya Kiti hiki cha Enzi!

141 Ninyi nyote mngetakaje kumwona ameketi kwenye Utukufu Wake? Hebu tufungue Ufunuo 21:10, upesi sana, na tumwangalie tu Yeye hapa. Vema, 21:10 hadi 11.

> *Akanichukua katika roho mpaka mlima mkubwa mrefu, akanionyesha* ule *mji mkuu, Yerusalemu takatifu, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu,*
>
> *Wenye utukufu wa Mungu:. . .Wenye utukufu wa Mungu: na* nuru *zake zilikuwa mfano wa kito chenye thamani nyingi kama. . .yaspi. . ., safi kama bilauri;*

142 "Nuru yake." Nuru! Ni nani aliye Nuru? "Nao huo Mji haukuhitaji jua, kwa kuwa Mwana-kondoo ndiye Nuru yake."

143 Jiwe la "yaspi, akiki." Utukufu wa Mungu ni Yesu Kristo, Utukufu wa Yesu Kristo ni Kanisa Lake. Naye alikuwa wa Kwanza. Alikuwa ni nini? Alikuwa ndiye Mwanzo wa wakati, Yeye ndiye Mwisho wa wakati. Alikuwa wa Kwanza wa wazee wetu, Yeye ndiye wa Mwisho wa wazee wetu. Alikuwa ndiye Kanisa lililokuwa katika. . .Alikuwa ndiye—ndiye Roho aliyekuwa katika Kanisa la Efeso, Yeye ndiye Roho wa Kanisa katika Laodikia. Yeye ndiye wa Kwanza na wa Mwisho, A hata Z, wa Kwanza, wa Mwisho, Yeye Aliyekuwako na Atakayekuja, Shina na Mzao wa Daudi, Nyota ya Asubuhi, Nyinyoro ya Bondeni, Ua la Uwandani! Loo, kuna sifa mia nne na kitu katika Biblia zinazomhusu Yeye. Wazia tu hilo, kile alichokuwa! Na hata hivyo alikuwa Bwana Yesu mnyenyekevu aliyezaliwa katika hori kwa sifa za Mungu.

144 Chochote kilicho kinyenyekevu, kiangalie maana hicho ni cha kweli. Chochote ambacho ni kikubwa kina kiburi, kwa

hiyo kamwe usikijali; unaona, ni upepo mwingi, wala hakina kitu. Vema.

145 Sasa, "Alionekana mithili ya jiwe la yaspi na akiki." Hebu tufungue. Mmeninii . . .? Tuna muda kidogo, sivyo? Tungali tuna kama dakika arobaini bado. Hebu tuone, hebu turudi katika Ezekieli 1. Rudini katika Biblia katika Agano la Kale, katika Ezekieli, na hebu tusome hapa ambapo Ezekieli alimwona, pia. Na tuyalinganishe Maandiko haya sasa tuone mahali tulipo. Ezekieli mlango wa kwanza, vema, sasa hebu tusome kwa dakika moja. Sasa nitasoma vifungu vitano vya kwanza, kisha tutasoma, nimevitia alama hapa, kutoka 26 hadi 28. Lakini hebu tusome vifungu vya kwanza sasa vya mlango wa kwanza wa Ezekieli, nabii. Vema:

> Tena *ikawa katika mwaka wa thelathini,* na *mwezi wa nne, siku ya tano ya mwezi,* . . . *nilipokuwa pamoja na watu waliohamishwa—pamoja na watu waliohamishwa, karibu na mto Kebari* . . . (Hiyo ni sawa, Kebari? K-e-b-a-r-i, Kebari.) . . . ndipo *mbingu zilifunuka, nikaona* ono *la Mungu.*
>
> Na *katika* . . . (Sasa, angalieni.) . . . *Siku ya tano ya mwezi, nao* ndio mwezi wa kuhamishwa kwake *mfalme Yehoyakini,*
>
> *Neno la Bwana lilimjia Ezekieli, kuhani, mwana wa Buzi, kwa dhahiri, katika nchi ya* . . . *Wakaldayo, karibu na mto* wa *Kebari; na mkono wa Bwana ulikuwa* . . . *juu yake.*
>
> *Nikaona, na tazama, upepo wa dhoruba ulitoka upande wa kaskazini,* . . .

146 Mwangalie nabii huyu hapa, miaka mia tano na tisini na mitano kabla ya kuja kwake Kristo, angalia jinsi ono lake linavyolingana na Yohana:

> . . . *upepo wa dhoruba ulitoka upande wa kaskazini, wingu kubwa sana,* . . . *moto,* ukijitokeza*, na mwangaza pande zote, na katikati yake* palikuwa na *kitu kama rangi ya kaharabu, katikati ya moto huo.*
>
> *Kukatokea katikati yake mfano wa viumbe hai wanne. Kuonekana kwao kulikuwa hivi: walikuwa* na *sura ya* . . . *mwanadamu.*

147 Angalieni, rangi ya Roho wa Mungu iliyokuwa juu ya mfano wa hawa Viumbe wanne, ilikuwa ni kaharabu. Kaharabu ni manjano-chanikiwiti. Sasa, angalieni, "manjano-chanikiwiti," *kaharabu,* loo, Yeye ni yule yule jana . . . Yeye alijifunua Mwenyewe kwa Ezekieli; katikati ya ono la Ezekieli, Nuru hii aliyoiona ikija juu ya hao Wenye uhai wanne ilikuwa ni manjano-chanikiwiti. Alipomjia Yohana, alimtokea katika *zumaridi* ambayo pia ni "manjano-chanikiwiti." Anakuja sasa

kwa mfunuzi katika manjano-chanikiwiti. Anatujia sisi katika manjano-chanikiwiti, ile Nuru! Tembeeni katika Nuru, Yeye ni Nuru.

148 Hebu twende kwenye kifungu cha 26 sasa, tupate kusoma hadi cha 28. Kifungu cha 26:

> *Na juu ya ang-. . .*

Loo, mtakapofika nyumbani, ninawatakeni mtie hilo alama mkasome kila sehemu yake. Kuokoa wakati:

> *Na juu ya anga lililokuwa juu ya vichwa vyao, palikuwa na mfano wa* jiwe, *kuonekana kwake kama jiwe la* yakuti *samawi: na juu ya mfano huo wa kiti cha enzi, ulikuwako mfano* kama *kuonekana kwa mfano wa mwanadamu juu . . . yake.*

149 Huyo alikuwa ni Mwana wa Adamu, mnaona, Kristo. Sasa angalieni jinsi alivyokuwa, jinsi alivyovikwa hapa:

> *Nikaona kama kwamba ni* rangi *ya kaharabu,* (angalieni, kumzunguka huyu Mwana wa Adamu) *kama kuonekana kwa moto ndani yake* pande *zote—ndani yake pande zote, tangu kuonekana kwa viuno vyake . . .*

150 Sikilizeni! Iweni wa kiroho, iweni wenye kufahamu, na mioyoni mwenu wenyewe hapa. Ninawaapisha katika Jina la Yesu, msimwambie mwingine jambo hili! Ila kumbukeni tu jinsi lilivyo na baraka!

151 "Nika-. . ." Hebu tuanzie tena kwenye kifungu cha 27. Sikilizeni, kila mmoja! Iweni wa ufahamu kabisa sasa!

> *Nikaona kama kwamba ni rangi ya kaharabu* (hiyo ni manjano-chanikiwiti), *kama kuonekana kwa moto ndani yake . . .* pande *zote,* (Moto kuzunguka kaharabu-chanikiwiti. Sasa:) *tangu kuonekana kwa viuno vyake na juu,* (Tangu viuno vyake kwenda juu.) *na tangu kuonekana kwa viuno vyake . . . chini, naliona kama kwamba ni kuonekana kwa moto, tena palikuwa na mwangaza* pande zake *zote.* (Moto pande zote.)
>
> *Na kuonekana kwa upinde wa mvua,* na *katika* rangi *katika* siku *za mvua, ndivyo kulivyokuwa kuonekana kwa mwangaza ule* pande *zote. Ndivyo kulivyokuwa kuonekana kwake* na *mfano huo wa utukufu wa* B*WANA*. *Nami nilipoona nilianguka kifudifudi, nikasikia sauti ya mmoja anenaye.*

152 Angalieni! Mko tayari? Sikilizeni! Wekeni hili sasa, kumbukeni tu, kuwajulisha. (Gene, unaweza kuishikilia kanda hii.) Sikilizeni! (La, si lazima niishikilie hapo, hilo ni sawa. Ninamaanisha iweke tu hiyo kanda; iruhusu hii kwa Kanisa.) Angalieni hili! Sasa, mpate kujua kwamba rangi ya Nuru iliyo na Bwana, na Nuru ya Bwana inayomfuata Bwana, na ni kama Bwana, ni kaharabu, manjano-chanikiwiti. Hiyo ndiyo Nuru ile

ile iliyo nasi leo hii, kama vile wanasayansi walivyoipiga picha, manjano-chanikiwiti, kaharabu.

153 Wakati nikiwa mvulana mdogo, nami nimeiona kwa mara yangu ya kwanza, mnakumbuka, watu wa zamani hapa. Daima niliwaambia kabla ile picha halisi kupigwa, "Ilikuwa manjano-chanikiwiti, ambayo ni kaharabu." Sasa, kuwafanya mjue ya kwamba Roho wa Bwana . . .

154 Yeye alisema, alipoiona kutoka kwenye viuno vya Kiumbe hai kilichosimama mbele zake, "Tangu kiunoni mwake kwenda juu ilikuwa ni kama moto, Nuru tangu kiunoni kwenda chini, kulifunikwa na Nuru. Pande zote kulikuwako na rangi nyingi kama upinde wa mvua." Hiyo ni kweli?

155 Ninawatakeni kukumbuka, Mungu angali anapatikana katika rangi zizo hizo, "tangu viunoni kwenda juu, moto, rangi ya kaharabu," iliyopigwa kwa kamera ya sinema ama kamera ya rangi, "kaharabu tangu viunoni kwenda juu, tangu viunoni kwenda chini, pande zote, rangi nyingi kama zilivyo kwenye upinde wa mvua angani baada ya mvua." Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele! Roho Mtakatifu angali katika nguzu Zake, angali Kanisani Mwake katika siku hizi za mwisho. Haya basi. Sio mimi, nilikuwa tu nimesimama pale, bali ni picha iliyopigwa. Ninawatakeni mwiangalie hiyo, kile hasa Ezekieli alichoona. Rangi zile zile, kwa njia ile ile, na akatenda vile vile, na kumulika vile vile, juu ya wale Wenye uhai. Ni kitu gani? Wale Wenye uhai wanawakilisha Kanisa hai, Kanisa linaloishi kwa nguvu na kufufuka kwa Kristo. Rangi zile zile za kaharabu zimelifunika tangu viunoni kwenda juu, tangu viunoni kwenda chini.

156 Hakuna kubahatisha tena, sayansi imezipiga hizo picha! Angalieni rangi zao, angalieni tu rangi za moto humo ndani. Mnaona? Upinde wa mvua. Angalieni hii rangi ya manjano-zumaridi. Sasa, kwenye kamera *hii*, ilikuwa ni picha ya kawaida tu ya kamera ya mpiga picha. Kwenye kamera *hii* kulikuwako na rangi, picha za rangi, rangi ya Kodachrome. Angalieni hizo rangi za zumaridi mle ndani. Laiti ningeweza kuiweka kwenye nuru mahali fulani ambapo mngeweza kuona mkiwa huko nyuma. Mnaweza kuona sasa? "Kama upinde wa mvua," angalieni miale ikija huku na huku kama upinde wa mvua, kila moja rangi tofauti. Tutalifikia hilo katika dakika chache, hizo rangi ni nini na zinaonyesha nini?

157 Loo! Hilo linaufanya tu maskini moyo wangu kuruka kwa furaha. Na kujua ya kwamba katika siku hizi tunazoishi, kwamba Kristo . . . wakati sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao, sakafu zingine zote. Nafikiri, "Kwa nini nisiweze kuelezea hilo? Kwa nini siwezi kuufanya ulimwengu ulione?" Ulimwengu haukukusudiwa kuliona. Ulimwengu hautaliona,

kamwe hawataliona! Bali kanisa linapokea mtikiso wenye nguvu kuliko wote lililopata kuwa nao!

158 Katika siku hizo wasingeweza kupiga picha Yake. Wanaweza sasa kwa sababu wana vyombo vya kimitambo. Wale wanaojaribu kuichukua mitambo wapate kumkana Mungu, wanarudi moja kwa moja na kuthibitisha Mungu yupo. Hiyo ni kweli, "Zumaridi." Sasa, kumbukeni, kamwe mimi sikujitungia hilo, ninawasomeeni moja kwa moja kutoka katika Biblia. Angalieni ninaposoma, na mwangalie, na muone ya kwamba ni Bwana Mungu yeye yule, hakuna tofauti. Angalieni kifungu cha 27:

> *Nikaona. . .rangi ya kaharabu*, *kama* katika *kuonekana kwa moto*. . .

159 Mnaona, kama miali ikiwaka. Mnaona? Rangi za kaharabu zikitoka kwenye moto. Mnaliona sasa? Kaharabu, *hii* ni rangi ya kaharabu ikitoka katika moto. Hapa chini inasema:

> Na *kuonekana* kama *upinde,* ama upinde wa mvua *ulio katika siku* baada ya *mvua,*. . .upinde wa mvua, *katika* siku baada ya *mvua,*. . .

160 Na kulikuwako na—na "Kiumbe hai." Kile Yohana alichowakilisha, Kanisa zima, lilitwaliwa juu. Niliwaambia. Mtu mmoja hapa katika ono anaweza kuwakilisha Mwili mzima wa Kristo, kufunikwa! Sasa, angalieni:

> *Nikaona. . .kwamba ni rangi ya kaharabu, kama kuonekana kwa moto. . .pande zote* kwake, na *kuonekana. . .tangu kuonekana kwa viuno vyake na juu, na tangu kuonekana kwa viuno vyake na chini, naliona kama kwamba ni kuonekana kwa moto*. . .

161 Tazameni, *angalieni* moto ukienea. Kutoka kwa kitu gani? Upinde wa mvua, zile rangi saba. Sasa, angalieni, kuna rangi saba hasa *pale,* nao upinde wa mvua una rangi saba.

> . . .*naliona kama kwamba ni kuonekana kwa moto, tena palikuwa na mwangaza* pande zake *zote*.
>
> *Kama kuonekana kwa upinde wa mvua, ulio katika* mawingu *siku ya mvua*, *ndivyo kulivyokuwa kuonekana kwa mwangaza ule* pande *zote*. (Pande zote kukizunguka Kiti cha Enzi cha Mungu, mnaona.) *Ndivyo kulivyokuwa kuonekana kwake mfano huo wa utukufu wa* B*WANA*.

162 Sio *Bwana*, sasa, *utukufu wa* Bwana. Utukufu wa Bwana ukilifunika Kanisa Lake kwa sababu Yeye yuko ndani ya Kanisa Lake! Amina! Loo, linasikika ni la kijinga kwa wasio na hekima, bali jinsi lilivyo kuu kwa wale waaminio. A-ha.

> . . .*Ndivyo kulivyokuwa kuonekana kwake* na *mfano huo wa utukufu wa* B*WANA*. *Nami nilipoona nalianguka kifudifudi, nikasikia sauti ya mmoja anenaye*. . .

163 Sasa yeye anaendelea na kuelezea maana ya hilo ono, ambalo hatuna wakati wa kulifikia asubuhi ya leo.

164 Sasa, angalia jinsi Bwana katika neema Yake kuu ametupa mambo haya.

165 Sasa hebu tumchukue mwingine. Ezekieli na Yohana pia walimwona katika siri za rangi Zake na Nuru, na kuiita "rangi ya kaharabu." Yohana baadaye. . . Ninyi ambao huandika. . . mnayaandika Maandiko, Yohana wa Kwanza 1:5 hadi 7. Yohana, baadaye (naye alikuwa katika kisiwa cha Patimo yapata miaka mitatu wakati alipokiandika Kitabu hicho), wakati aliporudi, mzee wa miaka tisini na kitu, katika Yohana wa Kwanza 1:5 na 7, yeye alisema, "Mungu ni Nuru." Yohana alikuwa na tukio, alikuwa amemwona na alijua Yeye alikuwa ni Nuru, Nuru, Nuru ya Milele; si nurulimwengu, si nuru ya taa, nuru ya umeme, nuru ya jua, bali Nuru ya Milele! Loo, jinsi ninavyompenda. "Mungu ni Nuru."

166 Angalieni, tutarejea nyuma sasa tuone mahali tulipo. Tungali bado kwenye kifungu cha 3, sivyo? Tutakipata? Natumaini. Vema:

> . . . *yeye*. . . *alionekana* mithili ya *jiwe la yaspi na* akiki: *na upinde wa mvua*. . . *ulikizunguka kile kiti cha enzi, ukionekana mithili ya zumaridi.* (Manjano-chanikiwiti.)

167 Sasa, "upinde wa mvua," mnaona ulikuwa ni upinde wa mvua. Hebu turudi kwenye Mwanzo 9 tuone, katika Mwanzo 9:13. Nasi tutaona hapa nyuma "upinde wa mvua," wakati upinde wa mvua ulipotokea kwa mara ya kwanza. Mwanzo mlango wa 9, na tutaanzia kwenye kifungu cha 13, Mwanzo 9:13. Nyote mnalipenda Hili? Loo, ninalipenda! Silifurahii tu, ninalipenda mno! Angalieni:

> *Mimi naweka upinde wangu* mawinguni, *nao utakuwa ni ishara* (Angalieni!), *ishara ya agano* kati *yangu na nchi.*

168 Ati nini? "Kati Yangu na Nuhu"? La. "Kati Yangu na nchi."

> *Hata itakuwa, nikitanda mawingu juu ya nchi, upinde utaonekana winguni:*
>
> *Nami nitalikumbuka agano langu, lililoko—lililoko* kati *yangu na ninyi*. . .

169 Sasa anarejea kwenye agano Lake kati yao, bali lile agano la upinde wa mvua. . . Mnaona, hilo agano lilikuwa uhai kwa Nuhu, kwamba Yeye alimwokoa, bali lile agano ambalo Mungu alifanya na Nafsi Yake lilikuwa ni upinde wa mvua, kwamba Yeye asingeninii. . . Sasa, nitawaonyesha kile agano la Nuhu pamoja na Mungu lilichokuwa, katika dakika moja. Bali hili hapa lilikuwa ni Agano la Mungu Mwenyewe pamoja na Nafsi Yake, Amina, upinde wa mvua.

170 Sasa, tunaona ya kwamba *agano* basi ni "ishara," ishara. Mungu alisema lilikuwa ni "ishara" hapa, sivyo? Mnaona?

> *Mimi . . . naweka ninii yangu . . . Mimi naweka upinde wangu* winguni, (Hiyo ni baada ya maangamizi ya ulimwengu, ulioangamizwa kwa maji; wote wenye mwili, mbali na Nuhu—Nuhu, waliangamizwa.) *nao utakuwa ni ishara ya agano kati yangu na nchi.*

171 Sio "Mimi na ulimwengu." *ulimwengu* ni "kosmosi." Mnaona? Bali hili ni "kati yangu na nchi." Mungu alisema, "Niliumba dunia hiyo. Nami niliisihi vibaya sana, hata nikaipindua juu chini tu na kuivunja vipande-vipande. Na—na ha—ha—ha—ha—haikunipasa kufanya hivyo, labda." Kasema, "Ha—hata nilijuta, lilikuwa ni jambo la kutisha sana."

172 Unafikiri itakuwaje atakapokuja katika hasira Yake sasa? Kuwa sawa, ewe rafiki mwenye dhambi.

> Loo, kesha ukingoja kuiona tamasha hiyo,
> Yeye yuaja tena. (Mnaamini hilo?)
> Yeye yuaja tena. (Napenda hilo, nanyi je?)
>
> Loo, ungehesabiwa kama mmoja wa adui Zake? (Nisingetaka kuwa hivyo. Nawe je? La bwana. Kuwa adui dhi- . . . Ama, kuwa adui Wake; kuwa pamoja Naye kungekuwa sawa. Lakini dhidi Yake . . .)
> Kuwa bila waa kwa ndani, uwe ukikesha na kungojea kuiona tamasha hiyo,
> Yuaja tena. (Hmm!)

173 Sasa, agano, ishara ya nini? Ishara ya nini? Ya sadaka ambayo imekubalika. Sasa fungueni Mwanzo 8:20 na 22. Sasa, Mwanzo 8:20 na 22, vema, moja kwa moja upande wa pili wa ukurasa.

> *Nuhu* akamjengea *BWANA madhabahu; akatwaa . . . kila mnyama aliye safi, na . . . kila ndege aliye safi, akavitoa sadaka za kuteketezwa juu ya madhabahu.*
>
> *BWANA akasikia harufu ya kumridhisha; BWANA akasema moyoni, Sitalaani nchi tena* (kulaani nchi), *baada ya hayo kwa sababu ya wanadamu; maana mawazo ya moyo* wa *mwanadamu ni mabaya tangu ujana wake; wala sitapiga tena baada ya hayo kila kilicho* hai *kama nilivyofanya.*

174 Na sasa tunaweza kusoma kifungu cha mwisho:

> Na . . . *Muda nchi idumupo, majira ya kupanda na mavuno, . . . baridi na joto, . . . kiangazi na masika, . . . mchana na usiku, havitakoma.* (Agano.)

175 Jambo lile lile ambalo Yohana aliona: Yesu, agano la Mungu lililokubalika likizizunguka mbingu. Na karibu na Yeye kulikuwako na upinde wa mvua pande zote za Kiti cha

Enzi, ulioonekana mithili yake kama zumaridi, Mwangaza wa kaharabu-chanikiwiti pande zote za Kiti cha Enzi. Mungu apewe sifa!

176 Angalieni! Wa Nuhu ulikuwa hasa sana. . . Upinde wa mvua wa Nuhu ulikuwa hasa sana wa rangi saba. Mtu yeyote anajua upinde wa mvua una rangi saba. Sasa, rangi hizo ni zipi? Nyekundu, chungwa . . . urujuani. La, nyekundu—nyekundu, chungwa . . . chanikiwiti, samawati, nili, na urujuani. Hizo ndizo rangi za upinde wa mvua. Sasa, tuna jambo la kilindi hapa, nami itanibidi tu kugusia sehemu zake muhimu maana wakati unaenda sana. Sasa, kumbukeni, chungwa . . . ama, nyekundu, chungwa, manjano, chanikiwiti, samawati, nili, na urujuani.

177 Sasa, kama mkiangalia, saba. Angalieni. Pinde saba za mvua . . . rangi saba, namaanisha, upinde wenye rangi saba. Hiyo ilimaanisha pinde saba! Pinde saba, makanisa saba yakiakisi taa saba, kila taa imefunganishwa katika nyingine. Ilianza na nyekundu, nyekundu. Baada ya nyekundu ikaja ya chungwa, ambayo ni uakisi wa nyekundu. Baada ya chungwa ilikuwa . . . baada—baada ya chungwa inakuja manjano, ambayo ni nyekundu na chungwa zikichanganywa pamoja, zinakuwa manjano. Kisha kijani kibichi. Kijani kibichi na samawati zinafanya nyeusi. Kisha inakuja nili. Ndipo kutoka kwenye nili inakuja urujuani, ambayo ni sehemu ya samawati. Haleluya! Hivi hamwoni? Mungu, katika upinde Wake wa mvua wenye rangi saba, agano Lake alilofanya, agano ambalo kupitia kwenye Nyakati Saba za Kanisa, zile rangi saba, Yeye angeiokoa dunia.

178 Angefanya nini? Kumbukeni, Yeye alilifanya na dunia, rangi Yake. Lakini sasa angalieni. Upinde huu wa mvua pekee, kimlalo, hufunika tu (katika upinde) nusu dunia. Hiyo tu ndiyo upinde wa mvua wa Nuhu ulitia rangi, ninii tu . . . ulifunika, nusu tu ya dunia. Ulikuwa ni katika tao, hiyo tu ndiyo unayoweza kuona. Lakini wakati Yohana alipomwona *Yeye* katika rangi Yake ya zumaridi, Yeye alikizunguka Kiti chote cha Enzi cha Mungu. Nusu haijasimuliwa bado. Yeye alifunika . . . Alininii tu . . . dunia inafanya tu tao, ni nusu yake tu; hizo ni nyakati za kanisa.

179 Lakini wakati Yohana alipomwona katika rangi Yake ya zumaridi, rangi ya kaharabu, alizungukwa na kufunikwa kama duara ya nuru. Duara ya nuru! [Ndugu Branham anatulia na kugongagonga kitu fulani kuonyesha—Mh.] Duara ya nuru ya rangi ya kaharabu, iliuzunguka utu Wake! Mnaona? Rangi moja, Mungu mmoja juu ya wote, kupitia kwa wote, na ndani ya wote, bali kuna Nyakati Saba za Kanisa.

180 Angalia almasi kuu. Walikuwa wakizipata . . . unaweza kuzipata Afrika zikiwa barabarani. Usithubutu kuweka moja, maana haijakatwa. Ukiwa na moja ambayo haijakatwa,

watakushtakia hiyo sasa hivi, na kukupa kifungo cha maisha kwa sababu ya kuiweka. Ukiipata, ilete mara unapoipata.

181 Sasa, wanachukua almasi hii. . . Loo, ni kitu kigumu. Nimeona mashine kubwa ya kusagia ya tani arobaini imesimama *hivi*, wanaweka hilo jiwe la samawati mle ndani, inalisaga, inalipondaponda jiwe hilo kama tu majivu, bali haitaiponda almasi. Tani hizo arobaini zikining'inia kwenye ekseli, *hapa* juu, ikibingirika pamoja na hayo magurudumu makubwa namna hiyo, ikilivunja tu hilo jiwe vipande-vipande; bali almasi itapitia moja kwa moja humo, itasogeza chuma hicho cha tani arobaini. Loo! Inapoponda na kupitia kwenye chujio, inachuja vichujio vingine, inaoshwa halafu hatimaye inapitishwa kwenye njia ndefu.

182 Meneja wa Machimbo hayo makuu ya Almasi ya Kimberley alikuwa mmoja wa mabawabu wangu huko chini mstarini, ndugu mnyenyekevu sana, wa kupendeza.

183 Halafu kwa yapata futi tatu juu ya maji hayo, mahali yanapotiririkia, ni, ni Kosmolaini imewekwa pale. (Mnajua, m—mnakiitaje kitu hicho? Ninii. . . Meda, ni kitu gani kile tulicho nacho kwenye kabati mle ndani? Vaselini!) Nasi tunaweka hiyo Vaselini, yapata kilindi cha inchi moja, huku juu kabisa kwenye mtelezo. Nayo inatelemka, na angalia, kila wakati jiwe hilo linapopita hapo, litateleza moja kwa moja kwenye Vaselini hiyo; bali wakati almasi inapopitia juu yake, itanata. Almasi ni kavu na itanata kwenye hiyo. Nimewaona wakiziokota, hata hizo ndogo sana, na kuzitenganisha kwa miwani. Nami nikawauliza ni kwa nini walikuwa wakifanya hivyo, wakasema huziuzia Marekani kwa ajili ya sindano za santuri za Victrola na kadhalika; hazichakai, mnaona.

184 Lakini hizo almasi kubwa, sasa, hizo hapo, mpira mmoja mkubwa tu. Lakini wakati. . . Wanazichukua na kuchukua mitambo ya umeme na kuzikata, na kufanya almasi iliyokatwa. Ndipo wakiisha kuzikata, ni kuakisi rangi zinazowaka moto za karati yake, na itaakisi rangi saba, pia.

Loo, jinsi ambavyo Yesu. . .

185 Loo, huenda ukawa na pesa nyingi sana, huenda ukawa na msururu wa Makadilaki, huenda ukawa mchungaji wa nyumba kuu ya maiti ama kanisa kuu la kitu fulani, huenda ukawa askofu ama askofu mkuu, bali, loo, ndugu, utakapokipata Kito hicho, hiyo Almasi, mtu huuza mali yake yote aliyo nayo, na kuitoa, na kadhalika.

186 Mwangalie yule mwanamwali aliyelala. Loo, yeye alifanya nini? Ilimbidi kuuza kitu fulani kusudi anunue Mafuta yake. Ilimbidi kuuza nini? Maskini kanuni zake za imani na madhehebu na kadhalika. Aliuza yote aliyokuwa nayo kusudi ampate Kristo, Kristo, kile Kito kikuu. Yesu, ule mwili. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . .? . . . Nina tikiti

ya kwenda Mbinguni wakati garimoshi litakapokuja, moja ya asubuhi hizi zenye giza. Loo, ni baraka jinsi gani!

> Loo, jinsi bubujiko hilo lilivyo la thamani
> Linalonifanya mweupe kama theluji;
> Sijui chemchemi nyingine,
> Ila Damu Yake Yesu.

187 Hakuna umaarufu, hakuna mambo makuu, hakuna kitu, hakuna utajiri, hakuna—hakuna kitu, nipe tu hilo Bubujiko la thamani. Hivyo tu!

> Sina cha mkononi niletacho,
> Nashikilia tu Msalaba Wako.

188 Kito hicho kikuu! Kilikuwa ni kitu gani? Kilikuwa kamilifu. Kilikuwa kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu na nusu hapo Mungu alipokipitisha kwenye ule mtambo mkuu wa kuponda, wakati alipokipeleka kule na kuanza kukitengeneza. Alikikata, akakiponda-ponda, akakijeruhi.

> *. . . alijeruhiwa kwa makosa yetu, . . . akachubuliwa kwa* uovu *wetu: adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake; na kwa kupigwa kwake sisi* tuliponywa.

189 Mungu alimfanyia nini Mtu huyo mkamilifu? Kuna mmoja wao tu ulimwenguni, mmoja tu ulimwenguni, na huyo alikuwa ni Yeye! Naye Mungu akamkatia hapa, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu." Kwa sababu nilikuwa mwenye dhambi, Yeye aliacha Mwangaza wa upinde wa mvua wa Nyakati Zake Saba za Kanisa unimulikie, nipate kujua ya kwamba alijeruhiwa kwa makosa yangu.

190 Huo hapo upinde wako wa mvua wenye rangi saba. "Alichubuliwa kwa makosa yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Mungu alimkata, akamjeruhi, akamponda, na kumkata, ili aweze kuakisi kupitia kwa majeraha Yake yaliyokuwa yakifa, msamaha wa dhambi, furaha, amani, subira, wema, upole, unyenyekevu. Zile Roho saba za Mungu ni matunda saba ya Roho ambayo yangeakisi kwa watu Wake. Yeye alijeruhiwa, akatengenezwa na kufanywa, kusudi Nuru ya Mungu ikiangaza kupitia mwili wa Mtu huyo mmoja iweze kuukomboa ulimwengu mzima; "Nitainuliwa juu ya nchi, nitawavuta watu wote Kwangu." Angalieni hizo pinde za rangi zinapoakisi.

191 Lakini wakati Yohana alipomwona hapa, ilikuwa ni nini? Siku ya ukombozi ilikuwa imekwisha. Yote yalikuwa yamekwisha, kwa hiyo alimwona amerudi kwenye hali Yake ya asili, rangi ya kaharabu. Sio tu nusu ya ulimwengu, linaweza tu . . . jua, linaweza tu kuangaza juu ya nusu ulimwengu kwa wakati mmoja, mnaona, linapozunguka. Lakini wakati Yohana alipomwona, alikuwa ameketi akionekana mithili ya jiwe la yaspi na akiki, rangi za kaharabu; zichanganye hizo mbili pamoja, unapata kaharabu. "Na rangi ya kaharabu pande

zote za Kiti cha Enzi!" Loo, jamani! Loo, na—nawaambia, hilo linaninii tu . . . tungeweza kuendelea mbele zaidi na zaidi.

192 Roho saba, rangi saba, nyakati saba za kanisa, wahudumu saba, taa saba, kila kitu kiko katika saba. Mungu amekamilika katika "saba." Mungu alifanya kazi siku sita; siku ya saba, akapumzika. Ulimwengu utadumu miaka elfu sita, nayo elfu ya saba ni ule Utawala wa Miaka Elfu.

193 Angalieni, *katika nusu duara,* "nusu haijajulikana." Sasa, hakika mambo haya yanawakilisha kitu fulani.

194 Sasa, katika Kutoka 23:13 na katika Waebrania 6:12, Mungu alifanya agano na nafsi Yake na kuapa kwa nafsi Yake. Waebrania :13 inatwambia kwamba, ama 9, :13, kwamba "Aliapa kwa nafsi Yake." Hapakuwapo na mkubwa zaidi wa kuapia hapo alipomwambia Ibrahimu na Isaka, hapo alikuwa amemwambia Ibrahimu ya kwamba angefanya agano naye, agano la milele. Mungu . . .

195 Agano daima hufanywa kwa kiapo, kwa hiyo hapakuwapo na mtu . . . Unaapa kwa mtu aliye mkubwa kuliko wewe; unaapa kwa mama yako, unaapa kwa taifa lako, unakula kiapo kwa kitu fulani, unaapa kwa Mungu. Bali huwezi kuapa isipokuwa iwe ni mtu aliye mkubwa kuliko wewe.

196 Wala hapakuwapo na mkubwa kuliko Mungu, kwa hiyo Yeye aliapa Mwenyewe, kwa nafsi Yake. Amina! Kuapa kwa nafsi Yake ya kwamba angethibitisha agano hili. Amina. Loo! Whiu! Akaapa kwake, kwamba Yeye "ataudumisha Uzao wa Ibrahimu." Uzao wa Ibrahimu ni nini kwa Mataifa? Ubatizo wa Roho Mtakatifu, Uzao wa Ibrahimu. Akaapa kwa nafsi Yake, "Nitawainua, kila mmoja, juu. Nitawapa Uzima wa Milele na kuwaweka tena hapa duniani." Tuna nini cha ku- . . . cha kuwazia?

197 Kwa hiyo tunamwona kwenye upinde mduara wa rangi ya kijani kibichi, kaharabu. Hii ya kijani kibichi, kijani kibichi kinawakilisha nini? Uhai. Kijani kibichi ni isiyokauka, sikuzote ni kijani kibichi, ni uhai. Inamaanisha nini? Ya kwamba Mungu ameahidi, kwa kuwa aliapa huko katika Mwanzo, ya kwamba Yeye "asingeninii . . ." (Akaweka upinde wa mvua angani.) kwamba Yeye "hatauangamiza ulimwengu huu kwa maji tena." Yeye pia hula kiapo na kuapa kwa nafsi Yake ya kwamba atafufua Wazao wa Ibrahimu wote, na ulimwengu huu utakabiliwa na hukumu zote zake za kutikiswa. Zile hukumu tutakazopitia kwenye masomo yajayo ya usoni, zitawaonyesha ambapo ulimwengu huu utateuka na kugeuka volkeno, na kulipuliwa vipande-vipande, na juu chini na kila kitu. Lakini Yeye huapa kwa nafsi Yake ya kwamba hatauangamiza, bali ataupiga msasa tena na kuwaweka watoto Wake duniani kwa ajili ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Loo, jamani!

Ninatazamia kule kuja kwa ile Siku ya furaha ya ule Utawala wa Miaka Elfu,
Wakati Bwana wetu mbarikiwa atakapokuja kumchukua Bibi-arusi Wake anayengojea;
Loo! moyo wangu unatamani, ukiililia ile siku ya kuwekwa huru kutamu,
Wakati Mwokozi wetu atakaporudi duniani tena.

198 Loo, jinsi tunavyotamani kuiona Siku hiyo, Yeye aliahidi ule Utawala Mkuu wa Miaka Elfu ungekuja. Na jambo lingine, sababu ya Yeye kuzungukwa, Yeye ni Mungu anayetimiza agano. Atatimiza agano Lake!

199 Sasa hebu tukiendee kifungu kinachofuata, kwa vyovyote vile. Jamani, tunataka kuchukua kingine kimoja, nasi tuna karibu tu dakika kumi, kumi na tano kufanya hivyo. Mmechoka sana? Mnataka kuendelea? [Kusanyiko linasema, "Amina!"—Mh.] Vema, hebu tuchukue kifungu cha nne:

> *Na viti ishirini na vinne* vilikizunguka *kile kiti cha enzi: na juu ya vile viti naliona wazee ishirini na wanne, wameketi, wamevikwa mavazi meupe; na juu ya* vichwa *vyao walikuwa na taji za dhahabu.*

200 Huenda tusipitie kwenye kifungu hicho chote. Vema, hebu tuanze. Kifungu cha 4, angalieni sasa, wakati Yohana alipomwona, ile rangi ya zumaridi imemzunguka, tulipata rangi hizo zote, pinde za mvua, na kadhalika, na yale hayo yote yalihusu. Sasa, kwenye kifungu cha 4, jambo la kwanza analozungumzia hapa, kwenye ninii cha 4 . . .

> *Vilikizunguka kile kiti cha enzi . . .*

201 Angalieni! Ni picha nzuri sana hapa, msiikose, "kile Kiti cha Enzi."

202 Mwajua, hebu turudi nyuma kwa Musa. Musa . . . Hatuna wakati wa kulichambua, kwa hiyo chukueni tu kile ninachosema. Musa, wakati alipopewa ono juu ya Mlima Sinai . . .

203 Ninataka muone ya kwamba hiki hakikuwa ni Kiti cha Enzi cha neema tena. Hapo, damu ilikuwa imekwisha, na dhabihu ilikuwa imerudi tena nao walikuwa wamekubalika, nayo damu haikuwako kwenye kiti cha rehema. Basi sasa kilikuwa ni kiti cha hukumu kwa kuwa ngurumo na radi zilitoka kwake. Hiyo ni kweli?

204 Kumbukeni, ilikuwa ni kama Mlima Sinai. Wakati Musa alipopanda Mlima sinai, nini kilitukia? Ngurumo, radi. Na hata kama ng'ombe au ndama au kondoo, au yeyote yule, hata akiugusa ule mlima, hana budi kufa. Biblia ilisema, "Tetemeko la nchi lilikuwa kubwa sana hata Musa akaliogopa." Naye Mu- . . . Akasema, "Vua viatu vyako hapa, uko mahali

Patakatifu." Yoshua yule shujaa hodari, aliyekuwa awavushe hao watoto na kuwagawia urithi wao, angeweza kufika tu nusu ya mlima huo.

205 Hapa alisimama Musa kule juu huku rangi za Mungu zikimulika na radi na zumaridi zimemzunguka, akiangalia zile amri zikiandikwa. Amesimama mbele za Mungu, ile Sauti ikimjibu, "Musa, uko wapi? Vua viatu vyako, umesimama mahali Patakatifu."

206 Kiti cha hukumu, kilikuwa hivyo sasa, hakuna kitu kingaliweza kusimama hapo ila waliokombolewa. Mwenye dhambi asingaliweza kukikaribia hata kidogo (imekwisha), kile kiti cha hukumu. Vema.

207 Sasa, Musa alifanya vitu duniani, akaifanya maskani, kama vitu alivyoviona Mbinguni. Tunajua hilo, sivyo? Tunaona Paulo alifanya jambo lile lile. Hapana budi . . . Waebrania 9:23, kwamba Musa alifanya vitu kama tu alivyofanya. Naye Paulo katika ono lake wakati alipopaa Mbinguni (wakati alipokifundisha kile Kitabu kikuu cha Waebrania), hapana shaka aliona katika ono lake kitu kile kile alichoona Musa, kwa sababu alisema ya kwamba (alikifundisha Kitabu kile cha ajabu cha Waebrania), jinsi ambavyo Ukristo ulikuwa ndio mfano wa Agano la Kale. Yeye alikuwa ni mwalimu mkuu, Mu- . . . Paulo alikuwa. Sasa, hicho kilikuwa ni Kiti Chake cha Enzi *wakati huo*. Halafu katika . . .

208 Hebu tuninii tu . . . Hakuna haja, siwezi . . . Nilikuwa nikitaka kuruka hili, bali siwezi kamwe kuliruka. Ubao uko wapi? Uliurudisha? Umerudishwa, Doc? Vema, labda ninaweza kuwafanya mlione kutoka hapa. Ni—ni . . . Sasa, chukueni penseli zenu na karatasi, kwa kuwa ninataka kusema jambo fulani hapa. Ni—nilikuwa nimeketi asubuhi ya leo wakati kitu fulani kiliponijia. Sasa nitawaambieni kile nilichofanya, kama mkiangalia, nimelichora nyuma ya hapa. Mnaona? Nilichora tu sawasawa na vile Roho alivyonipa, mnaona, nikachora hapa jinsi ingekuwa. Ila ni—ninataka kusema jambo fulani papa hapa.

209 Sasa, Mungu, wakati ameketi kwenye kiti cha enzi, Yeye ni Hakimu basi. Hiyo ni kweli? Hakimu hutoa hukumu lini? Anapokuja kwenye kiti chake cha hukumu, kiti cha enzi. Sasa, ninawatakeni mwangalie jinsi Agano la Kale lilivyofanywa, jinsi nyua zilizokikaribia kiti Chake cha Enzi zilivyofanywa, na jinsi Yohana alivyoona hapa. Hatutalifikia asubuhi ya leo, yote. Lakini vile Yohana alivyoziona nyua zile zile za kule kumkaribia Yeye, na jinsi kuzikaribia nyua Zake kulivyo. Sasa, loo, napenda hili.

210 Sasa, katika Agano la Kale, kulikuwa na kile kilichoitwa "kusanyiko," ambapo watu walikusanyika. Jambo la kwanza, kabla ya kuingia, kusanyiko, kuingia mle, ilibidi waje chini

ya damu iliyomwagika, nyua za nje. Kwanza walikuja kwenye maji ya farakano, ambapo ndama mwekundu alichinjwa na kufanywa maji ya farakano. Huyo ni mwenye dhambi anayekuja na kulisikiliza Neno.

211 Hivyo ndivyo huyu rabi mkuu wa Kiyahudi alivyoletwa kwa Bwana, alinisikia nikihubiri juu ya hilo huko ninii . . . huko Tulsa. Huko Tulsa, ndiko ilikuwa. Tulikuwa huko Tulsa, Oklahoma. Naye akaja pale, mtazamaji tu. Naye akaenda baada ya ibada, akasema, "Ninajua!" Kasema . . . Yeye ni mmoja wa marabi saba walio hodari sana ulimwenguni. Basi alikuja kule, kasema, "Ninataka kuona kile hao Wafanyabiashara Wakristo . . . Wanawaita, 'Wapentekoste.' Ninataka kwenda kule, niketi chini, nisikilize."

212 Na wakati Bwana aliponifanya kuzungumza juu ya dhabihu ya ndama mwekundu, baada ya ibada alikutana na baadhi ya ndugu kule nyuma, kasema, "Ningetaka kukutana na mtu huyo. Ninajua ya kwamba hata hana elimu lakini . . . " Kasema, "Mimi ni rabi wa Kiyahudi anayejua mitazamo hiyo yote mbalimbali na vitu kama hivyo," kasema, "sijawahi kuona hilo maishani mwangu mwote." Kasema, "Sijawahi kuliona."

213 Na sasa yeye ni rabi Mpentekoste, aliyejazwa na Roho Mtakatifu, akienda kila mahali, akihubiri Injili. "Rabi Mpentekoste," ndivyo anavyojiita. Alienda kwenye Hoteli ya Washington Youree, hivi majuzi wakati tulipokutana huko kwa Ndugu Jack, naye mama huyo alimfahamu, akasema, "Rabi," kasema, "tuna chumba kizuri kwa ajili yako, ila," kasema, "hatujaweka televisheni mle."

214 Akasema, "Hivyo vitu ni 'kuzimuvisheni,' vitupeni nje! Sivitaki hapo ndani, kwa vyovyote vile; vingalikuwa hapo ndani, ningewafanya mvitupe nje."

Akasema, "Rabi!"

Akasema, "Mimi ni rabi Mpentekoste." Haleluya!

215 Kasema, "Sasa, utakapoenda Israeli, Ndugu Branham, ninataka kwenda pamoja nawe." Kasema, "Tunaweza kuipelekea watu wetu."

216 Nikasema, "Sio sasa, Rabi, sio sasa. Sio sasa, wakati haujawadia bado, ngoja kidogo."

217 Sasa, tazameni mahali hapa patakatifu. Sasa, unapoingia kwenye hizi nyua, pa kwanza palikuwa ni nyua, nyua za nje. Pa pili palikuwa na madhabahu, ambapo sadaka ilitolewa, madhabahu ya shaba. Halafu nje ya madhabahu ya shaba, kulikuwako na pazia lililoning'inizwa hapa lililoingia kwenye Patakatifu pa patakatifu; mle ndani mlikuwamo na kiti cha rehema, mle ndani mlikuwamo na Makerubi. Hilo ndilo ninalotaka kuendea katika somo letu lijalo, hao Makerubi

wanaokifunika kiti cha rehema. Loo, jamani! Mimi . . . Tunaweza tu kukaa mwezi mzima juu yake, juu ya huyo Kerubi.

218 Sasa, sasa angalieni wakati wakiingia ndani. Kusanyiko lingeweza kuja *pale*; makuhani wangeweza kusimama *hapa*; bali kuhani mkuu ndiye tu angaliweza kuingia *pale*, mara moja kwa mwaka, akibeba damu.

219 Naye ilibidi avalie kwa njia fulani, vazi fulani; ilibidi awe na kengele na komamanga, moja kwa nyingine. Na alipotembea, ilibidi atembee kwa njia fulani. Wakati akitembea, alicheza, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana," hizo kengele na komamanga zililia pamoja, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu!" Kwa nini? Alikuwa akimkaribia Mungu, akiwa na damu ya agano mkononi mwake, ikienda mbele Zake, akibeba damu.

220 Ametiwa mafuta (Loo, jamani!) kwa manukato fulani. Ilibidi nguo zake zishonwe na mkono uliojazwa na Roho Mtakatifu, mikono iliyosajiliwa ishone nguo zake. Ua la Uwandani, mafuta ya kupaka, yakamiminiwa kichwani mwake, yakatiririkia kote kwenye ndevu zake halafu mwilini kwa manukato ya kifalme; komamanga na kengele; akiichukua damu ya mwana-kondoo asiye na hatia; wala hathubutu kulikaribia hilo pazia nje, angefia papo hapo, alipokuwa amesimama. Kwa hiyo ilimbidi aende, akitembea kwa njia fulani, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu," (akimkaribia Mungu) "kwa Bwana. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu!"

221 Basi alienda pale na kutoa damu kwenye kiti cha rehema, mara moja kwa mwaka. Na wakati akiwa mle, alijaliwa kuuona Utukufu wa Shekina; wakati ile Nguzo ya Moto, ile Nuru ya kaharabu iliyoshuka, iliyowaongoza wale wana kutoka Israeli. Hata alilitia hekalu moshi hata hakuna mtu angeweza kuliona. Utukufu wa Bwana ulishuka mpaka lote likajaa moshi. Ndipo akaja Mwenyewe, akaingia nyuma ya pazia na kutulia juu ya kiti cha rehema katika Patakatifu pa patakatifu. "Mahali Patakatifu zaidi," panaitwa, Patakatifu pa patakatifu. Naye ilimbidi avalie kwa namna fulani, atembee kwa njia fulani, atiwe mafuta kwa njia fulani. Yeye alikuwa ni mtu maalumu kuingia mle. Jinsi ambavyo kusanyiko hapana shaka lilimwonea wivu!

222 Bali Yesu alipokufa, pazia la hekalu lilipasuka. Sio tu kuhani mkuu, bali "yeyote atakaye" anaweza kupata upako ule ule wa Utukufu wa Shekina na kutembea maisha matakatifu, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana," na kuukaribia Uwepo wenyewe wa Mungu, kwa Damu ya Yesu Kristo mbele zake. Anaenda pamoja na: "Bwana Yesu, huyu hapa mtu mgonjwa, yeye ni ndugu yangu. Yuko kwenye kitanda cha mauti sasa hivi, apate kufa. Ninakukaribia Wewe, 'Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana.'"

"Kwa sababu gani?"

"Kama kuhani mkuu."

"Kwa sababu gani?"

"Kwa niaba ya ndugu yangu. 'Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana.'"

223 Haya basi! Matembezi yako ya kila siku, mazungumzo yako ya kila siku, matendo yako ya kila siku, moyo wako, nafsi yako, na yote, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana." Hakuna shina la chuki, hakuna chochote kingine, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana," tunapoanza kukaribia kwa niaba ya ndugu yetu. Atakaye na aje, ametiwa mafuta, Damu ikiwa mbele yake, Damu ikimtangulia, akicheza "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana."

224 Sasa, hizo zilikuwa ni nyua za nje, mahali patakatifu. Na Patakatifu pa patakatifu, hayo yalikuwa ni madhabahu ya Mungu duniani. Angalieni, yalifananishwa na yale ya Mbinguni. Sasa, tutarudi moja kwa moja tena kwenye Andiko lili hili. Loo, yote tunapopitia kwenye Ufunuo, tunaweza kurejea moja kwa moja kwenye hili tena. Mnaona?

225 Sasa yeye. . . Yohana, Yohana anasimama wapi? Kwenye zile nyua. Hebu tusome mbele kidogo tu hapa kusudi mwipate picha yake:

> *Na katika kile kiti cha enzi* kunatoka *umeme*. . . ngurumo. . .*sauti: na taa saba za moto* (Ngojeni mpaka tutakapozifikia hizo!) *zikiwaka mbele ya kile kiti cha enzi, ndizo Roho saba za Mungu.*

226 Zikiakisi Nuru ya Mungu Kanisani, moja kwa moja kutoka katika Kiti cha Enzi cha Mungu, sio kupitia kwenye seminari, sio kupitia kwa askofu fulani, bali kutoka kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, kwa ufunuo wa nguvu za kufufuka Kwake, zikimfanya Yeye yule yule jana, leo, na hata milele; hizo nyota saba zikisimama pale zikiakisi Nuru hiyo, Nuru ya Shekina, kutoka kwenye Utukufu wa Shekina kutoka Patakatifu pa patakatifu. Taa saba za moto, zimewekwa juu ya hivi vinara vya taa, zikiakisi Nuru Yake, rangi Zake, za nguvu Zake za kufufuka Kwake, moja kwa moja Kanisani. Amina! Hmm!

> *Na mbele ya kile kiti cha enzi*. . .*kulikuwa na mfano wa bahari ya kioo* kama *bilauri: na katikati ya kile kiti cha enzi, na* pande zote *za kile kiti, walikuwako wenye uhai wanne, wamejaa macho mbele na nyuma.*

227 Naye anaendelea mbele na kuanza kutoa. . .hawa wenye uhai, sawa na wale Ezekieli aliowaona; hao walinzi. . .mmoja kama mwanadamu, mmoja kama simba, na mmoja kama tai. Ilikuwa ni kitu gani? Sasa, tazameni, tunapowaingiza na kuonyesha huyo Simba wa Kabila la Yuda na hao wote

mbalimbali kutoka kwa makabila yao, walioketi kwenye kuta nne, nao walikuwa wakikilinda kiti hiki cha rehema. Loo, ni picha ya jinsi gani! Loo, ninaninii tu. . . Kuna siku kuu zilizo mbele.

228 Kama tulivyowaona, sasa, hicho kilikuwa ni Kiti cha Enzi cha Mungu Mbinguni, Musa alikitengeza kwa mfano duniani, kilikuwa ni Kiti cha Enzi cha Mungu kwa sababu kiti Chake cha hukumu kilikuwa kimewakilishwa hapa duniani katika Patakatifu pa patakatifu. Mungu . . . Israeli wote walikuja mahali hapo pamoja kupata rehema, maana Mungu alikutana tu chini ya damu iliyomwagika.

229 Sasa, sikilizeni kwa makini. Ndipo Utukufu wa Shekina ukainuka kutoka kwenye kiti hicho cha rehema siku moja, nao ukatulia kwenye Maskani nyingine (Amina!), Hii, "Baba hamhukumu mtu yeyote bali amempa Mwana hukumu yote." Kiti cha Hukumu cha Mungu. Whiu! "Ukinena dhidi Yangu, utasamehewa," ukinena juu ya mwingine—Mwingine anayekuja, Kiti kingine cha Rehema. "Ukinena . . . ukinena neno dhidi ya Mwana wa Adamu, nitakusamehe; bali siku moja Roho Mtakatifu atakuja kuishi katika mioyo ya watu, neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe."

230 Inaendelea kuwa kali zaidi na zaidi wakati wote, ile hukumu, maana Mungu anaendelea kuishiwa na saburi, akijaribu kuwafanya wenye dhambi waje Kwake wakapatanishwe. Kwanza, Yeye alikuwa mbinguni juu akiangaza kupitia nyota. Pili, alikuwa duniani akiangaza kupitia Utukufu wa Shekina. Halafu, akaja na kufanyika mwili akaishi miongoni mwetu, angali anamaliza saburi Yake. Kisha akawakomboa wanadamu kwa Damu Yake, akaingia Kanisani Mwake katika umbo la Roho Mtakatifu, na kunena dhidi ya Huyo ni jambo lililomalizika, limekwisha.

231 Sasa mnaweza kuona mahali kule kutikiswa kulikoingilia. Ambako wakati, hawatambui. Watu hawawezi kuelewa maana Yake.

232 Sasa, Kiti cha Enzi cha kwanza kilikuwa Mbinguni, kiti cha hukumu. Kiti cha Enzi cha pili kilikuwa katika Kristo. Kiti cha Enzi cha tatu kiko ndani ya mwanadamu.

233 Sasa, hebu nichukue kitu hiki kidogo ambacho nimechora hapa. Tutafanya . . . Laiti ningalikuwa na ubao wa kuandikia, ambao ningeweza kulifanya lieleweke vizuri zaidi kwenu. Tutachukua na kuchora nyua, kuzichora tu kama duara ya mviringo, au namna hii, mojawapo. Sasa tutachukua . . . Ninaamini, namna *hii* labda ingekuwa ni bora zaidi, tutachukua na kufanya nyua.

234 Sasa, mwanadamu ni nini? Yeye ni kiumbe cha sehemu tatu; mwili, nafsi, na roho. Ni wangapi wanaojua hilo? Angalieni njia ya kumkaribia Mungu. Moyo wake ni nini? Mnaukumbuka ule

ujumbe wangu, *Mungu Aliuchagua Moyo wa Mwanadamu Kama Mnara Wake wa Kuongozea*? Ibilisi alichagua kichwa chake kama mnara wake wa kuongozea; mnaona, anamfanya aone mambo, kuangalia kupitia macho yake. Lakini ndani yake... Mungu katika moyo wake humfanya aamini mambo ambayo hawezi kuyaona. Sivyo? Mnaona, Mungu yuko ndani ya moyo wake, ndani ya moyo wa mwanadamu kuna Kiti cha Enzi cha Mungu. Mnalipata? Mwanadamu! Mungu alifanya Kiti Chake cha Enzi katika moyo wa mwanadamu.

235 Sasa, angalieni. Sehemu ya kwanza ya mwanadamu ni nini? Sehemu ya kwanza ya mwanadamu ni *mwili*. Sehemu ya pili ni *nafsi* yake, ambayo ndiyo asili ya roho yake ambayo humfanya jinsi alivyo. Yeye anakaribia sasa. Sasa, sehemu ya tatu ya mwanadamu ni *roho* yake, nayo roho yake, ndiyo kiini cha moyo wake, na katika kiini cha moyo ndipo Mungu anapokuja kwa ajili ya Kiti cha Enzi.

236 Mnakumbuka, hivi majuzi, ma—magazeti yalitoa katika Chicago yapata miaka minne iliyopita, wakati maskini mwaminio...maskini asiyeamini, hasa, alikuwa akisema ya kwamba Mungu alifanya kosa kupitia kwa Sulemani wakati aliposema, "Jinsi mtu awazavyo moyoni mwake." Kasema, "Hakuna uwezo wa akili moyoni wa kuwazia. Angewezaje kuwazia kwa moyo wake? Inabidi aninii...Alimaanisha kichwa chake."

237 Kama Mungu angalimaanisha kichwa chake, Yeye angalisema, "kichwa chake."

238 Kama vile Musa, vipi kama Musa...Mungu angalisema, "Musa, vua viatu vyako, uko kwenye mahali Patakatifu"; aseme, "Vema, kwa nini nisitoe tu kofia yangu, hilo ni sawa vile vile"? Yeye alisema, "viatu." Hakusema, "kofia," alisema, "viatu."

239 Na wakati Yeye aliposema, "Tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo," Yeye hakumaanisha "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Alimaanisha tu kile Yeye alichosema.

240 Wakati aliposema, "Huna *budi* kuzaliwa mara ya pili," Yeye hakusema, "*Unapaswa*."

241 Yeye alisema, "Ishara hizi zi*ta*fuatana na hao waaminio," kamwe hakusema "*Labda* zitafuatana nao."

242 Yeye husema analomaanisha! Naye ni Mungu wala hawezi kulighairi. Yeye anajua kilicho kikamilifu kwa hiyo Yeye anakifanya namna hiyo, na hivyo ndivyo Yeye—Yeye anavyokikusudia kuwa. Nawe huna budi kukifikia Hicho. Sio Yeye ashuke aje kwenye wazo lako, inakubidi kupanda juu kulifikia Wazo Lake. Hiyo ndiyo tofauti.

243 Sasa, sasa, kwenye mfumo huu wa mwili, nafsi...Sasa, kama utachukua neno *nafsi* na kuliangalia, itakwambia katika—

katika kamusi ya Biblia ama Webster, mojawapo, ni "asili ya roho."

244 Sasa, huyu hapa mtu, tuseme, huyu *hapa* John Doe. Vema, John Doe. Na huyu *hapa* Sam Doe. Vema. Sasa, John Doe ni mwanadamu, mwili, yeye ni ndugu ya Sam Doe. Sasa, John ni roho, nafsi, mwili; naye Sam Doe ni kitu kile kile (mwili, nafsi, roho) kama yeye alivyo, mwili, nafsi, roho. Sasa, mtu *huyu* ni mwovu, katili, hudanganya, huiba, hulaghai, hufanya uzinzi, jambo lolote ovu analoweza kufanya; bali mtu *huyu* amejaa upendo, amani, furaha. Wote wawili wana nafsi, mwili, na roho. Vema, tofauti yake ni nini? Mtu *huyu* anaweza kurudi na kusema, "Ninamkumbuka mama yangu, ninakumbuka mambo tuliyofanya tulipokuwa wavulana"; wote wawili wanaweza. Wote wawili wana roho, wote wawili wana nafsi, wote wawili wana mwili.

245 Bali asili ya roho ya mtu *huyu* ni ovu; asili ya roho ya mtu *huyu* ni nzuri. Mnaona? Kwa hiyo asili ya roho ndiyo nafsi ya mwanadamu. Mnaona? Kwa hiyo, sasa, Mungu anajaribu kuingia ndani ya nini? Roho na moyo wa mwanadamu. Roho hukaa moyoni.

246 Mnajua, nayo sayansi ilisema (kwa kuwa sikumaliza hilo), kwamba mwanadamu asingeweza kuwaza kwa moyo wake. Ndipo sayansi ikaanza kugundua kwamba kuna sehemu ndogo katika moyo wa mwanadamu (sio katika moyo wa mnyama, bali katika moyo wa mwanadamu), isiyo hata na seli ya damu, wala chochote kile. Walisema, "Hapana shaka ndipo mahali ambapo nafsi inakaa, ama roho." Waache—waacheni tu, watavichukua vitu vyao vya kipumbavu na kumthibitisha Mungu. Hiyo ni kweli. Mungu huwafanya wapumbavu kumshuhudia.

247 Sasa, hiyo hapo, vichwa vikubwa magazetini. Msichana mdogo wa Ndugu Boze alisema, "Ndugu Branham, unajua kile ulichokuwa ukisema hivi majuzi?" Kasema, "Angalia, angalia, sayansi tayari imekiona."

248 Kasema, "Vema, Mungu abarikiwe! Ninataka hilo, dada, nataka—nataka hilo."

249 Nafsi ya mwanadamu ndiyo asili ya roho, nayo roho inakaa ndani ya moyo wa mwanadamu.

250 Sasa, sasa, nyua za nje ni nini? Hizo ni mwili. Mnaona? Hicho ndicho kitu cha kwanza unachofikia, mwili. Huna budi kuumaliza huo kwanza. Huna budi, kupita zaidi ya mwili. "Si—sijisikii kuamka na kwenda kanisani, barabara zinateleza sana. Na—na . . . Kuna joto kupita kiasi. Loo, kanisa, sijui." Huo ni mwili. Vema. Sasa, huna budi kuumaliza na kuupita huo, Mungu hana budi kupitia huo.

251 Wakati mwingine Yeye ajapo, hana budi kuingia kwenye nafsi, hiyo ni asili yake. "Loo, akina Jones watasema nini kunihusu mimi? Loo, jamani! Mwajua, kanisa langu litanifukuza

kama—kama nikifanya kitu kama hicho. Mnaona?" Bali huna budi kwenda uipite hiyo.

252 Na unapokwenda kuipita hiyo, basi Yeye anaingia moyoni na hapo ndipo Yeye anapoketi kwenye kiti cha enzi. Huyo ni Roho Mtakatifu ndani yako. Yesu alisema, "Ingekuwa bora zaidi kwamba jiwe la kusagia lifungiwe shingoni mwako na utoswe kwenye kilindi cha bahari, kuliko hata kumkosesha mmojawapo wa wadogo hawa wanaoniamini Mimi." Msiwadhuru hata kidogo; hata kuwakosesha, kuwaudhi tu kuhusu jambo fulani. Ingefaa sana wewe ungalizamishwa baharini, ama hukuzaliwa duniani, kuliko hata kumkosesha mmojawapo. Je, Yeye alimaanisha hilo? Angeweza kusema uongo? Mitume walisema hilo? La, la. Yesu alililisema! Yesu alisema, "Kama hata ukimkosesha mmojawapo, hawa watoto wadogo wanaoniamini Mimi."

"Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio!"

253 Jamaa mkubwa, mnene mno anasema, "Loo, ninamwamini! Haleluya!"

254 "Je, umewahi kunena kwa lugha, kufasiri lugha, kutoa pepo, maono, na kadhalika, kama Yeye alivyoahidi?"

"La, siku hizo zimepita." Yeye si mwaminio, yeye ni anayejifanya mwaminio.

255 Yesu alisema, maneno ya mwisho aliyosema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, ulimwenguni kote na kwa kila kiumbe." Hiyo ni kweli. "Zitafuatana na mwaminio hata nitakaporudi." Hayo ndiyo maneno ya mwisho aliyosema. Ni wangapi wanaojua hilo? Biblia, Marko 16.

Sasa, mnaona, Yeye ni anayejifanya mwaminio.

256 Lakini unapompata mwaminio ambaye kweli anaamini, pamoja na ishara zinazofuata, na unaona unyenyekevu wa maisha yao, sio mwigaji, jua kwamba hao ni Wakristo, mtu halisi, wa kweli, tulia tu. Jambo unalopaswa kufanya, ni kujiunga nao moja kwa moja, uanze kusonga mbele, maana unapitia moja kwa moja kwenye barabara kuu ya Mfalme.

257 Sasa, ni jambo gani linalotukia? Angalieni hili. Nyua za nje: zilikuwa ni wakati wa Luther, tunapoanza kwenye Mwili wa Kanisa la Kimataifa.

258 Mnakumbuka, walikuwa ni Wayahudi mpaka kufikia wakati wa—wa A.D. 606 wakati ilipofikia kwenye Thiatira, karibu wote walikuwa ni waongofu wa Kiyahudi. Lakini baada ya Wayahudi, ilishuka hapa kwenye Wayahudi na Wamataifa pia (bali zaidi sana ni la Kiyahudi). Bali kweli inapofikia kwenye wakati wa Kimataifa, inapofikia upande huu, mnaona, wanakuja Martin Luther, John Wesley, na kadhalika. Mnaona?

259 Sasa, waangalie hawa watatu baada ya ule Wakati wa Giza, wakaja mpaka kwenye Wakati wa Katikati na kuvuka.

Wakati unapokuja, angalieni hizi nyua za nje. Mnaona: mwili, nafsi, roho. Mnaona? Nyua za nje, mwili. Mahali patakatifu: Wanazarayo, Pilgrim Holiness, Methodisti Huru. Mnaona? Na Patakatifu pa patakatifu: kurudi katika Pentekoste, mahali ilipoanza hapo mwanzo, mnaona, kurudi hata mwanzo.

260 Sasa, kama mnachora, ninataka kutia alama. Sasa, yapo malango matano yanayoingia kwenye mwili, yanayoudhibiti mwili. Mnajua hilo. Sivyo? Hiyo ni zile hisi tano. Ni hisi ngapi zinazoudhibiti mwili? Tano: kuona, kuonja, kuhisi, kunusa, kusikia. Hiyo ni kweli? Huo ni mwili, nyua za nje, hivyo ni vitu usivyoweza kutegemea kwa sababu ni mwili.

261 Nyua za ndani basi, tuna nyua za ndani, ambazo ndizo madhabahu inayofuata. Nayo madhabahu nyingine inakuja, nayo inakuja na—na dhamiri, dhana, kumbukumbu, hisia kali, na upendo. Hizo ndizo zile hisi tano zinazodhibiti nyua za ndani. Hiyo ni nafsi. Hisi za upendo, hiyo ni nafsi, upendo, na kadhalika. Halafu inayofuatia kwenye kipimaji hiki hapa ndani, kuna pia kumbukumbu, na dhamiri, na rehema, na kadhalika, na—na—na dhana. Unaketi na kuwazia mambo, unafanya nini? Hufanyi hivyo katika mwili wako, hisi zako haziwazii. Ni ua wa ndani ulio ndani yako.

262 Ina milango mitatu. Tunafanya nini? Tunavunja sasa, msilikose. Kutoka kwenye mwili, zile hisi tano; kwenye hiyo nyingine, nafsi, nyua za ndani; lakini sasa unaingia kwenye moyo. Unaona?

263 Sasa, hapo ndipo ninyi Wapilgirm Holiness na Methodisti wazuri mlipokaa kwenye madhabahu hiyo *huko* nje. Mnaona, mko kwenye zile nyua. Ninyi Walutheri na kadhalika mmerudi kwenye mwili, huko nyuma pamoja na zile hisi tano, yale macho yanayoweza kuona na kutambua. Mnaona?

264 Hawa hapa Wapiligrim Holiness wanakuja ambao walikuwa tu ni Methodisti Huru, wakaja kwenye nyua za pili na kuamini katika utakatifu, maana paliitwa mahali patakatifu ambapo dhabihu iliwekwa.

265 Lakini mara moja kwa mwaka kuhani mkuu aliingia katika Patakatifu pa patakatifu ambapo palihukumiwa. Huo ulikuwa ni wakati wa Kilutheri; halafu wakati wa Kimethodisti; halafu wakati *huu*, mwangaza wa Kanisa ukija, ambao unafanana na mfumo wa mwanadamu.

266 Basi tu—tunaingiaje kwenye *hili*? Sasa, kumbukeni, kulikuwako na pazia, pazia linaloning'inia kati ya mahali patakatifu na Patakatifu pa patakatifu. Katika Patakatifu pa patakatifu ndipo Kristo anapokuja na kuketi kwenye kiti cha enzi cha moyo wako, Kristo anatawazwa. Anapitia kwenye kutakaswa (Hiyo ni kweli?); kutakaswa; "Halafu kwa ninii moja. . ." (maji. . .kwa kanisa moja. . .kwa kununi moja ya imani. . .La!) "kwa Roho mmoja," kutoka hapa sote tunabatizwa

kuwa Mwili mmoja ambao ni Mwili wa Kristo. Kwa kitu gani? Roho Mtakatifu.

267 Ni nani anayeingia? Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, Wapentekoste, kila atakaye. Pazia hilo, unajua ni nini pazia hilo linaloufunika moyo wako kutoka Kwake? Mko tayari? Hilo pazia linaitwa "hiari." Mnaipata hiyo picha sasa? Zile hisi *huko* nje, zile hisi kwenye mwili na hisi za nafsi, na lile pazia kati ya hizo na mahali patakatifu, Patakatifu pa patakatifu. Na jinsi tu unavyoweza kuingia mle ni kuwa na hiari yako! "Kwa maana yeyote. . . " Kitu gani? Kila anayepeana mikono? Kila anayezamishwa majini? Kila anayejiunga na kanisa? Kila anayepitisha barua yake? Kila afanyaye. . .? La! "Kila *atakaye* na aje ng'ambo ya pazia."

268 Hebu Kristo aje kwenye hizo hisi; useme "Vema, ninapaswa. Sitaki kwenda jehanamu, hilo ni jambo moja. Nitajiunga na kanisa." Vema, Mlutheri.

269 "Vema, nitawaambia nini, ninaamini ya kwamba ninapaswa kuishi maisha tofauti, niwezayo," utakaso madhabahuni. Vema, Methodisti.

270 Vema, halafu yeyote *atakaye*, na apite kwenye pazia lililopasuliwa. Loo, utukufu kwa Mungu! Niko upande ule mwingine. Haleluya kwa Jina Lake! Loo, jamani! Yeyote atakaye, na ayararue, mapazia ya mapenzi yake mwenyewe, na amruhusu Mungu aingie moyoni mwake. Huyo hapo Kristo juu ya kiti Chake cha hukumu katika moyo wa mwanadamu! Itakuwaje?

271 Unasema, "Sina budi. . .Loo, ni—ninaweza kufanya mizaha michafu, hainihukumu." Kwa nini? Hawana chochote kinachoweza kuhukumu. Hakuna Mtu mle ku—kuliondoa. Hakuna Mtu mle wa ku—kukuhukumu. "Vema, nitakwambia," wanawake wanasema, "Ninaweza kuwa na nywele fupi, hainihukumu." Si ajabu! Mnaona? "Loo, ninaweza kuvaa kaptura. . .Ninaweza kufanya *hili*. Mimi. . . " Wanaume walisema, "Hainidhuru kuvuta sigara, wala hainidhuru kucheza ka—karata na kutupa dadu," na lolote wafanyalo. "Hainidhuru." Nao wangali ni wafuasi wa kanisa, mnaona, "Hainidhuru kufanya *hivi*." Kwa nini? Kwa nini? Hakuna kitu mle cha kukuhukumu.

272 Bali Kristo anapoingia, umefanya madhabahu moyoni mwako na dhambi zako zinachukuliwa kila siku. Yule Mtakatifu mashuhuri Paulo, yeye alisema, "Ninakufa kila siku. Hata hivyo mimi ni hai, bali si *mimi* niishiye, Kristo yuaishi ndani yangu." Hiyo hapo pazia la ndani. Loo, ndugu, dada!

273 Kuharakisha, najua. . .Loo, la, mimi. . .kamwe siwezi kulimalizia, nimepitiliza wakati. Hebu tuone, hebu nininii tu. . . La, afadhali nisifanye hivyo. Mnaona, ninataka kuwachukua wale wazee ishirini na wanne, nami ninajua ninawacheleweshaW

nyinyi nyote kwa chakula chenu cha jioni. Tutaninii tu. . . Hebu tuone, kwamba. . .Ni wangapi wanaosema tuwachukue wale wazee ishirini na wanne? Ninii tu. . . [Kusanyiko linasema, "Amina!"—Mh.] Vema, hebu kidogo. Vema, hebu kidogo. "Wazee ishirini na wanne," basi, hebu tuwachukue upesi sana sasa, "wanaokizunguka kile Kiti cha Enzi, na walikuwa ishirini-. . . pande zote za kile Kiti cha Enzi."

274 Sasa mnaona kile. . .Kiti cha Enzi kiko wapi sasa? Moyoni. Katika moyo wa nani? Washiriki wa zile Nyakati Saba za Kanisa, Kristo! "Ukisema neno dhidi ya tendo lao, umehukumiwa," utawajibikia hilo kwenye Siku ya Hukumu. Na ni nani watakaoihukumu dunia? Watakatifu wataihukumu dunia.

275 Danieli aliona akina nani wakija pamoja na makumi elfu mara elfu kumi? Wakatakatifu. Vitabu vilifunguliwa, wenye dhambi. Kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni Kitabu cha Uzima, yule mwanamwali aliyelala. Loo, jamani, hivi hawawezi kuona hilo? Kanisa lililolala, wale waliotoka kwenda kumlaki Bwana-arusi, waliacha Mafuta yaishe kwenye taa yao; kamwe hawakuingia Humu, hawakumwacha Kristo achukue mamlaka ili aweze kufanya miujiza na kunena kwa lugha na kufanya maajabu na kadhalika kuthibitisha ya kwamba aliishi katika Kanisa Lake.

276 Vipi kama Yesu angalikuja duniani na kusema "Mimi ni Yesu, Mimi ni Mwana wa Mungu," asingefanya chochote, Yeye angesema tu "Ni—nitapanda hapa nikajiunge na kanisa"? Je, huyo angekuwa ni Mwana wa Mungu?

277 Yeye alisema nini? "Nisipozifanya kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi."

278 Loo, jamani! Mnaona? Mungu hujitangaza Mwenyewe, anapenda kufanya hivyo. Yeye ni Yehova. Anapenda kujitambulisha. Loo, nina furaha sana kwa jambo hilo. Naam, bwana. Amejitambulisha kwangu, ninajua amefanya hivyo kwako. Baadhi yenu ninyi vijana ambao ndio kwanza mwongoke, hata hivyo hamninii. . .huenda hamumjui Yeye katika nguvu na mambo makuu ambayo Wakristo wa siku nyingi hufanya, bali mnayakaribia moja kwa moja. Mnakuja moja kwa moja kwenye njia kuu ya Mfalme. Msininii. . . Endeleeni tu kuangalia na kusukuma kwa nguvu mwezavyo. Kimbieni, kimbieni, kimbieni upesi tu mwezavyo. Msisimame kwa chochote kile, endeleeni tu kwenda.

279 Kama vile maskini Dada Snelling alivyozoea kusema:

Ninakimbia mbio, mbio, mbio, ndio kwanza nifike;
Ninakimbia mbio, mbio, mbio, ndio kwanza nifike;
Ninakimbia mbio, mbio, mbio, wala huwezi kuketi chini.

Maskini mama huyo mkongwe, yuko kule leo hii.

280 Vema, sasa, na kulikuwako—kulikuwako na viti vya enzi na kunavyo, kuna ishiri-. . . kulikuwako na viti ishirini na vinne. Sasa, hao wangekuwa ni wangapi, ishirini na wanne? Ishirini na wanne. Vema:

> . . . *viti ishirini na vinne: na juu ya kile* kiti . . . *juu ya vile viti naliona wazee ishirini na wanne,* (kila mmoja kwenye kiti kimoja), *wamevikwa mavazi meupe; na juu ya vichwa vyao walikuwa na taji za dhahabu.*

281 Sasa, "wazee ishirini na wanne." Nataka muone kwamba hawakuwa Viumbe wa Kimalaika. Malaika hawahusishwi, Viumbe vya Mbinguni havihusishwi na taji na viti vya enzi. Mnaona, hawahusishwi kamwe, hao ni Malaika, kamwe hawakushinda. Kama mkiangalia baadaye kidogo, nyimbo walizoimba, na kadhalika, zilithibitisha kwamba hawakuwa. Mnaona? Waliimba wimbo wa ukombozi; kwa hiyo, Malaika hawahitaji kukombolewa. Mnaona? Vema. Bali hawa walikuwa ni watu waliokombolewa.

282 Mimi si . . . ninyi watu, sitakuwa na wakati wa kushika hili. Bali ninyi mnaoandika, kama mkitaka kujua kwamba walikuwa watu waliokombolewa, chukueni Mathayo 19:28, vema, 19:28, Mathayo, Ufunuo 3:21, halafu mfungue hayo, Ufunuo 20:4, Ufunuo 2:10, Petro wa Kwanza 5:2 na 4, Timotheo wa Pili 4:8. Hayo yatawafanya mjue ya kwamba wamekombolewa. Ninataka kupitia hayo asubuhi ya leo, mnaona. Nanyi mnaweza tu kuyachambua kwa majuma kadhaa, mnaona. Hao hawakuwa—hawakuwa Viumbe vya Kimalaika, hawakuwa Viumbe vya Kimbinguni, walikuwa watu waliokombolewa. Mnaona? Unaweza kuzingatia mavazi yao, jinsi walivyovikwa; mnaweza kuzingatia mahali pao, walichokuwa nacho; mzingatie nyimbo, zile walizoimba; na kujua ya kwamba hawakuwa Viumbe vya Kimalaika. Hmm.

283 Ninachukia kufikia hili, bali hebu tusome Andiko lingine moja. Sivyo? Vema. Hebu turudi kwenye Danieli 7, kwa muda mfupi tu, hapa nyuma, Danieli 7, na tusome tu Andiko hapa. Ninataka . . . kwa hiyo hili litawasaidia sana katika ujumbe uliosalia asubuhi ya leo. Nina hakika ya kwamba lita—litawafanya mjisikie vizuri zaidi mkiisha kulisoma hili na kuona hili, kuona kile Danieli, mlango wa 7 wa Danieli, na hebu tuanzie sasa kutoka kwenye . . . Danieli 7, hebu tuchukue mla- wa 9 . . . kifungu cha 9. Sasa, yasikilizeni mambo haya kwa makini sasa:

> Na . . . *Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja aliye Mzee wa siku ameketi,* mavazi *yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele* za *kichwa chake kama . . . sufu safi;* na *kiti chake cha enzi kilikuwa kama miali ya moto,* (Mnaona tena, inarudi kwenye ule

moto wa zumaridi.) *na magurudumu yake kama moto uwakao.*

Na. . .*Mto wa moto ukatoka ukapita mbele zake:* maelfu mara *maelfu wakamtumikia, na* makumi elfu *mara* elfu *kumi* (Hao hapo waliokombolewa wanakuja.) *wakasimama mbele zake:* na *hukumu ikawekwa, na vitabu* (vitabu, wingi) *vikafunguliwa.*

284 Sasa, angalia, hukumu hii iliwekwa. Mnaona? Sasa, angalieni. Danieli, wakati alipoviona viti vya enzi kwenye ile hukumu, vilikuwa vitupu, aliona "viti vya enzi vimewekwa, vikishushwa kutoka Mbinguni, aliye Mzee wa siku akashuka kutoka Mbinguni." Bali wakati Yohana alipokiona, Kiti hicho cha Enzi kilikuwa tayari kimekaliwa na Yesu, na viti vya enzi vya wanafunzi na wale wazee wetu, waliokombolewa, vilikuwa tayari vimekaliwa. Mnaona? Danieli alikiona miaka mia tano kabla ya wakati wa Kristo. Ndipo baada ya Kristo, inafanya miaka elfu mbili mia tano, naye Yohana alikuwa akiishi kwenye wakati utakaokuja, naye tayari alikuwa ameona haya yote yakitukia. Ambapo, Danieli hakuyaona, (Mnaona?) alimwona tu aliye Mzee wa siku akija; alimwona akija. Bali wakati Yohana alipomwona, kile Kiti cha Enzi kilikuwa kimekaliwa, mnaona, viti vya enzi viliwekwa pamoja na aliye Mzee wa siku, na Hukumu ikawekwa. Lakini wakati Yohana alipomwona, wale wazee walikuwa bado hawajachaguliwa katika wakati wa Yohana. . .ama wakati wa Danieli, bali walikuwa tayari wamekombolewa kwenye wakati wa mwisho. . .?. . .Loo jamani! Loo, hiyo si ni . . . Yeye si ni wa ajabu?

285 Kwa hiyo, Danieli 7, yeye. . .Danieli alifanya nini? Yeye alitangulia kuiona ile Hukumu, akaona viti vya enzi vilivyowekwa vilikuwa vitupu. Mnaona, vilipaswa kuwa vitupu. Kwa kuwa Yohana katika wakati wake, baada ya Kanisa lililonyakuliwa, vilikaliwa na wazee waliokombolewa. Hmm.

286 *Mzee* maana yake nini? Kama ukichukua neno *mzee,* nina yapata. . .fafanuzi hizi zote zilizoandikwa hapa chini, ninaziruka tu. *Mzee* linamaanisha "kiongozi wa mji" ama "kiongozi wa kabila." *Mzee*, "kiongozi wa kitu fulani." Kama vile ni—ningekuwa . . . Ndugu Neville sasa hivi ni mzee wa kanisa hili. Yeye ni nini? Yeye ni kiongozi wa kundi hili la mahali hapa. Mnaona? Naye meya wa mji huu angekuwa ni mzee wa mji huu; mnaona, mzee wa miji. Mnakumbuka huko nyuma katika nyakati za Biblia, wale wazee wa mji? *Mzee* linamaanisha "kiongozi wa mji" ama "kiongozi wa kabila."

287 Sasa, walikuwa ni wangapi? Ishirini na wanne, wazee ishirini na wanne. Hiyo ni kweli? Sasa . . . Loo, jamani! Ilikuwa ni nani? Wale mitume kumi na wawili na yale makabila kumi na mawili ya Israeli, wale wazee wetu kumi na wawili. Ninii. . .Sasa, tutalifuatilia moja kwa moja mpaka tuyafikie yale masomo

mengine, na kuthibitisha kwamba hilo ni kweli, kusudi ninyi, nina furaha kwamba mnayaandika sasa. Mnaona? Wale wazee wetu kumi na wawili na yale makabila kumi na mawili ya Israeli! Sasa, angalieni. Yesu alisema kwamba . . .

288 Petro aliuliza siku moja, kasema, "Tutapokea nini? Tumeacha baba, mama, mume, mke, watoto, kila kitu kingine, tumeacha kila kitu." Petro akasema, "Tumewaacha wake zetu, tumewaacha watoto wetu, tumemwacha baba na mama, makazi yetu na mashamba, kukufuata Wewe."

289 Yeye akasema, "Amin, amin nawaambia, ya kwamba mtaketi juu ya viti kumi na viwili vya enzi mkiyahukumu yale makabila kumi na mawili." Haya basi, hao ni waliokombolewa, wazee waliokombolewa.

290 Angalieni—mwangalieni Daudi akionyesha Kristo. Mnaona? Wakati Daudi alipokuwa akiingia mamlakani, jambo la kwanza, alikuwa na wakati mgumu sana kabla hajaingia mamlakani. Hata hivyo alikuwa na upako juu yake, naam, upako ulikuwa juu yake. Na watu wengi walifikiri "Yeye alikuwa ni haini tu, jamaa mdogo aliyekuwa tofauti, akijaribu kurarua kitu fulani." Bali kuna watu waliojua alikuwa mfalme ajaye, wakakaa moja kwa moja pamoja naye. Ndugu, ninamaanisha usingeweza kuwaondoa kwake, wakati wakiendelea.

291 Siku moja alisimama pale juu mlimani, akaangalia chini na kuona maskini mji wake mwenyewe alioupenda umezingirwa na adui. Basi akasimama pale na kukumbuka wakati alipokuwa mvulana mdogo, alikuwa akiwapitisha kondoo pale na kunywa maji hayo, yalikuwa ni maji halisi. (Tumeyazungumzia hapa si muda mrefu uliopita, *Maji ya Uzima*.) Naye yule pale, "Wazieni, nilinywea hayo."

292 Nayo shauku yake iliyo ndogo sana ilikuwa ni amri kwa mtu yeyote aliyekuwa naye. Ndugu, wawili wa hao watu wakanyakua panga zao na kupigana kupitia maili kumi na tano za Wafilisti, wakiwakatakata kulia na kushoto, wapate kumletea maji ya kunywa kutoka kwenye kisima hicho. Walijua alikuwa anakuja mamlakani. Naam, bwana. Wakati mmoja, mmoja wao, apate kumwokoa, aliruka ndani ya shimo na kumwua simba, peke yake. Walikuwa ni mashujaa wa vita. Basi wakati—wakati alipoingia mamlakani, mnajua yale aliyofanya? Alimfanya kila mmoja wao mtawala juu ya mji fulani.

293 Mnamwona Kristo hapo? "Yeye ashindaye atautawala mji." Washindi! Leo hii tunapoona ya kwamba Yeye anakuja mamlakani, Kristo atatawala katika ulimwengu huu. Ujerumani, na Marekani, na yote hayana budi kuanguka, kila taifa halina budi kuanguka. Falme za ulimwengu huu zimekuwa falme za Mungu wetu na za Kristo Wake, Nayeataziongoza na kuzitawala. Hiyo ni kweli.

294 Tunajua Yeye yuaja mamlakani, kwa hiyo shauku Yake iliyo ndogo sana ni amri kwetu! "Yeye ananitaka nimwakilishe katika Timbuktu ndogo ambako hakuna hata senti hamsini za pesa, ambako hakuna chochote, ama kundi maskini la watu," hiyo ni shauku. Amina!

295 "Si lazima upate wengi sana, si lazima ufanye *hivi,* nifanye tu kujua Yeye anataka kwenda." Amina. Hivyo tu.

296 "Kama anataka nifanye vinginevyo, nifanye tofauti," kama dada hawa na kadhalika, "kama akitaka nifanye jambo fulani, Mungu abarikiwe, ni majaliwa kwangu kufanya hivyo." Haya basi! Tunajua Yeye anakuja mamlakani, haidhuru ulimwengu unasema nini. "Kama ikinibidi kuweka kando kila mzigo na dhambi inizingayo kwa rahisi, nijalie nipige mbio kwa subira mashindano yaliyowekwa mbele yangu. Jalia nimwangalie Mwanzilishi na Mwenye kumalizia Imani yetu, Yesu Kristo." Yuaja mamlakani!

297 Hao "wazee," hao wazee ishirini na wanne. Vema. Kumi na wawili...Katika ufunuo, tunaliona hili. Katika Kitabu cha Ufunuo, yapata mlango wa 21, tunapata ya kwamba mji wa Yerusalemu ulikuwa na misingi kumi na miwili. Hiyo ni kweli? Nao ulikuwa na malango kumi na mawili, hayo yalikuwa ni matatu kwa kila upande, tatu nne ni kumi na mbili. Jinsi hasa ambavyo ile maskani ilivyokaa nyikani, kwa kuwa Yohana alisema vivyo hivyo hasa na kuona kitu kile kile ambacho Musa aliona wakati alipokuwa huko juu, kitu kile kile alichoona Paulo.

298 Na sasa tunaona ya kwamba ile misingi kumi na miwili ilikuwa ni majina ya mitume. Nayo hayo malango kumi na mawili yalikuwa na jina la kila kabila langoni. Jinsi tunavyoangalia hilo na kuona wale wazee kumi na wawili, yale makabila kumi na mawili, mitume kumi na wawili, ile misingi kumi na miwili, milango kumi na miwili! Loo, jamani! Hebu chukueni hizo numerali za Mungu na hamwezi kuzikosa mahali popote, zitaenda sambamba kabisa kila mahali kila wakati.

299 Hiyo ndiyo sababu, mnaona, tunazo siku hizi sita ambazo ulimwengu umeshughulika, nasi tuko karibu kabisa na hii siku ya saba sasa. Miaka elfu mbili ya kwanza, Mungu aliangamiza maji...ulimwengu kwa maji. Miaka elfu mbili ya pili, Kristo alikuja. Huu ni mwaka wa 1961, karibu sana mlangoni, muda mfupi tu. Pia angalieni, Yesu alisema, "Sasa, wote hautaendelea hata mwisho," Yeye alisema, "kwa kuwa itanibidi kuifupisha kazi. Nisipoifupisha, bomu la atomiki litawaangamiza wote wenye mwili. A-ha. Kwa ajili ya Wateule, nitaifupisha kazi katika haki. Kuifupisha, sehemu ya huo wakati." Mnaona, halafu ule Utawala wa Miaka Elfu, ile Siku kuu.

300 Wakati Kanisa limejitahidi dhidi ya dhambi kwa miaka elfu sita, nayo ya elfu saba ni ule Utawala wa Miaka Elfu. Kama vile

Mungu alivyotumia miaka elfu sita kuujenga huu ulimwengu, na elfu ya saba akapumzika kutoka kwa kazi Zake zote. Nalo Kanisa linajitahidi dhidi ya dhambi kwa miaka elfu sita, na elfu ya saba Kanisa linapumzika.

301 Mavazi meupe waliyovalia wale wazee ndiyo haki ya Watakatifu. *Nyeupe* inamaanisha "haki." Na kwa kuwa *walivikwa* mavazi inaonyesha ya kwamba walikuwa "makuhani au mahakimu," wenye mavazi meupe, makuhani, mahakimu, manabii, kadhalika; mnaona, kile walichokuwa. Walikuwa wamevikwa mavazi meupe, wale wazee ishirini na wanne. Kutakuwako na wazee ishirini na wanne. Kutakuwako na kumi na wawili wao kwa ajili ya makabila kumi na mawili ya Israeli; mitume kumi na wawili kwa ajili ya Kanisa.

302 Nao waliketi kwenye baraza za Mfalme mkuu. Kumbukeni, wameketi huko nje, *hawa* ndio. Naye huyu *hapa* Bibi-arusi pamoja na Kristo wameketi kwenye Kiti Chake cha Enzi, naye Mke Wake ameketi karibu Naye, Kanisa. Wale wazee ishirini na wanne... Wale matoashi mia na arobaini na nne elfu wa hekaluni wakimtumikia. Anaposimama, Mke Wake anaambatana Naye. Loo, loo jamani! Kupitia kwa ule Wakati mkuu unaokuja, wakati dhambi zote na mfano wa dhambi...

303 Mijengo yote mikubwa, mizuri ambayo watu wanaipenda sana siku hizi, fedha na tamaa mbaya na dhambi yote na wanawake warembo na wanaume, na chochote wanachojaribu kuifanya miili yao, chochote kile, kuwa mtego wa ibilisi kuzipeleka nafsi zao kuzimuni, itaangamia na kuoza, na mabuu ya ngozi yataila. Na jambo la kwanza, mabuu ya ngozi... yote waliyowahi kuwa yataingia tu katika moto wa volkeno irudi iwe si kitu ila mabaki ya mabomu na—na majivu ya volkeno.

304 Lakini moja ya asubuhi hizi, ewe rafiki, moja ya asubuhi hizi, wakati yote hayo yatakapokwisha, itachanua tena. Mashamba pamoja na maua yake meupe na ha—harufu nzuri ya waridi itachanganyana na maua kutoka kwenye Mti wa Uzima, na Kristo atarudi asubuhi moja. Wakati ndege wakubwa, hua, wataketi kwenye miti na kulia, na hakutakuwako na mauti tena wala huzuni. Kristo na Waliokombolewa Wake watarudi ardhini; sio wazee, bali vijana milele. Wasiopatikana na mauti, tutasimama katika sura Yake, tutang'aa zaidi ya jua na nyota.

Ninaelekea kwenye ule mji mzuri
Bwana wangu ameuandaa kwa walio Wake;
Ambapo wote waliokombolewa wa nyakati zote
Wataimba "Utukufu!" wakikizunguka Kiti Cheupe cha Enzi.
Wakati mwingine ninapatwa na shauku ya Mbinguni

Na utukufu tutakaouona huko juu;
Itakuwa ni furaha jinsi gani nitakapomwona Mwokozi wangu,
Katika mji ule mzuri wa dhahabu!

Jinsi ninavyotamani kumwona! Loo, nataka kumwona!

Ninaelekea kwenye ule Mji mzuri!

305 Yohana aliuona, kwenye kisiwa cha Patimo, ukishuka kama Bibi-arusi aliyepambwa kwa ajili ya mumewe. Utukufu wake ninataka kuuona, siku moja.

Ninataka kumwona, na kuuangalia uso Wake,
Hapo nikaimbe milele juu ya neema Yake ya kuokoa;
Kwenye barabara za Utukufuni hebu niinue sauti yangu;
Masumbuko yote yamekwisha, hatimaye niko nyumbani, nikashangilie milele.

306 Kule kuteleza na kunyiririka kwenye theluji, joto kidogo na shughuli za siku; laiti mke wangu na Mabel wangekuja huku na kuniimbia ule wimbo, kama ni—ningeweza, "Masumbuko ya safarini yataonekana kana kwamba si kitu, nitakapofika mwisho wa safari." Hiyo ni kweli.

307 Nakumbuka ule usiku nilipoondoka kanisani kuanza kazi ya uinjilisti, wakati nyote mlikuwa mkilia; hakuna mmoja wao aliyetuacha, karibu hivyo, labda wachache wenu hapa. Dada na Ndugu Spencer, na labda wa—wachache wa watu wa zamani waliondoka, wakati walipolia hapa. Lakini wakati Roho Mtakatifu aliposema, "Huna budi kwenda!"

308 Nami ninakumbuka mkutano wangu wa kwanza baada ya kuondoka kwa miezi kadhaa, Meda alishuka kuja Jonesboro, Becky alikuwa ni mtoto mdogo sana, akashuka kuja kwa garimoshi la Ukanda wa kale wa Pamba, iliwachukua siku kadhaa kufika huko. Nami nilikuwa nimesimama huko nje wakati alipoingia usiku huo. Tulijaribu kuingia kwenye chumba cha mikutano, umbali wa majengo matatu, polisi walikuwa wameilinda mitaa namna hiyo. Mitaa ilikuwa imejaa watu. Iliwabidi, walinipitisha mitaani na kuzunguka-zunguka nipate kuingia mahali hapo. Meda akasema, "Je, walikuja kukusikia ukihubiri, Bill?"

309 Nikasema, "La." Ndipo tukaimba:

Wanakuja kutoka Mashariki na Magharibi,
Wanatoka nchi ya mbali,
Kula pamoja na Mfalme wetu, kula kama mgeni Wake;

Jinsi wasafiri hawa walivyobarikiwa!
Wakiutazama uso Wake uliotukuka
Unaong'aa kwa upendo wa kiungu;
Washiriki waliobarikiwa wa neema Yake,
Watakaong'aa kama johari kwenye taji Yake.

Loo, Yesu yuaja hivi karibuni,
Majaribu yetu yatakwisha basi.
Loo, vipi kama Bwana wetu angekuja wakati huu
Kwa ajili ya wale walio huru na dhambi?
Loo, basi ingekuletea furaha,
Au huzuni na kukata tamaa kabisa?
Wakati Bwana wetu ajapo katika utukufu,
Tutamlaki hewani.

310 Amina! Loo, ninampenda! Lingekuletea huzuni na dhiki kuu, ama lingekuletea furaha? Wakati Bwana wetu atakapokuja katika utukufu, tutamlaki juu hewani. Tukiwa na mawazo hayo niani mwetu, na tuviinamishe vichwa vyetu. Bwana akipenda, nitaimaliza ibada hii wakati mwingine.

311 Baba yetu wa Mbinguni, loo, watakuja kutoka Mashariki na Magharibi, watakuja kutoka nchi za mbali. Ninawazia juu ya ule Unyakuo mkuu. Watu ambao nimewahubiria Afrika, India, na kote ulimwenguni, jinsi nitakavyouona uso wao tena. Wengi wao wakilia, wakienda kwenye ndege, wakiegemea kwenye nyua na kupiga mayowe na kulia. Ninawazia juu ya wakati ule walipoambatana na Paulo wakati mmoja, wakapiga magoti na kuomba. Yeye alisema, "Nina hakika hakuna mmoja wenu... wengi wenu hapa hawatauona uso wangu tena."

Bali watatoka Mashariki na Magharibi,
Watakuja kutoka nchi za mbali,
Kula pamoja na Mfalme wetu, kula kama mgeni Wake;
Jinsi wasafiri hawa walivyobarikiwa!
Wakiutazama uso Wake uliotukuka (katika Utukufu wa zumaridi)
Unaong'aa kwa Nuru ya Kiungu; (Sio tu mwangaza wa taa ama mwangaza wa mshumaa, bali—bali Mwangaza wa Kiungu, unaong'aa kwa Mwangaza wa Kiungu.)
Washiriki waliobarikiwa wa neema Yake,
Watakaong'aa kama johari kwenye taji Yake.

Ee Mungu!

Wakati kaa la Moto lilipokuwa limemgusa nabii,
Likimfanya safi iwezekanavyo,

Wakati sauti ya Mungu iliposema, "Ni nani
atakayekwenda kwa ajili yetu?"
Ndipo akajibu, "Mimi hapa, nitume mimi."

312 Loo, mtume Malaika asubuhi ya leo, Makerubi wenye mabawa sita, kama Isaya alivyowaona, wakiruka kupitia jengoni, wakilia, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana." Naye Isaya yule nabii kijana akasema, "Mimi ni midomo michafu, na miongoni mwa watu wachafu, nayo macho yangu yameuona Utukufu wa Bwana." Nguzo zilitikisika hekaluni. Ndipo Malaika akachukua makoleo kutoka madhabahuni, akachukua kaa la moto na kuliweka kwenye midomo yake, kasema, "Ninaisafisha midomo yako. Sasa tabiri, mwana wa Adamu." Mtume Malaika asubuhi ya leo, Bwana, isafishe midomo yetu na uovu wowote. Isafishe mioyo yetu, na uingie ndani, Bwana. Vunjilia mbali ukaidi. Ili kwamba . . . jalia mapenzi yangu (ndani Yako) yawe ndiyo Mapenzi Yako, Bwana. Loo, dhamiria Mapenzi Yako ndani yangu, Ee Mungu. Na unijalie mimi pamoja na kanisa langu na watu wangu kuwa wako, Ee Bwana. Tunajikabidhi Kwako.

313 Na kama vile mshairi alivyoendelea kusema, Baba:

Mamilioni sasa wanakufa katika dhambi na
aibu; (Huko Afrika, huko chini India, kote
ulimwenguni, maelfu kwa saa, na kukutana
na Wewe bila kukujua Wewe.)

Mamilioni sasa wanakufa katika dhambi na
aibu; (Hata hivyo, Mungu, inairarua nafsi
yangu vipande-vipande kuliwazia.)
Kisikie kilio chao cha huzuni na uchungu;
Hima, ndugu, hima kwa kimbilio lao;
Upesi jibu, "Bwana, mimi hapa."

314 Tujalie, Bwana, tujalie tena. Nimefanya kila namna ya makosa, Baba, kote katika mwaka huu uliopita, naomba unisamehe hayo. Na katika Mwaka huu Mpya, Bwana, nitie mafuta upya. Jalia niwaendee hao mamilioni wanaoketi huko katika dhambi na aibu, waonakufa, nikawaletee ufunuo huu mkuu wa Kweli Yako, nikiwaletea upako wa Roho Mtakatifu; ili kwamba kwenye siku ile waweze kuja kutoka Mashariki na Magharibi, wakinawiri kama johari katika Taji Yako. Nisaidie, Bwana, kushuka kwenda na kuwatafuta na kuwachimbua kutoka ardhini, mavumbi ya ardhini, mavumbi na uchafu wanaoishi ndani yake. Na uwajalie wamwone Mungu Mtakatifu anayewafanya wajisafishe na kuishi kama Wakristo, waliotakaswa na safi mbele Zako; wakiuondokea uovu, kutokana na raha zote za kilimwengu, na kumgeukia Mungu aliye hai, na kuwafanya wajumbe wa Ufalme Wako kwa ajili ya ile siku kuu.

315 Litakase kanisa hili dogo asubuhi ya leo, Bwana. Mtakase kila mtu aliye humu ndani kwa Roho Wako, na jalia Roho Mtakatifu aingie mioyoni mwao, kila mmoja wetu. Ifanye upya Roho iliyo ndani yao ambao tayari wame-. . .wameifungua mioyo yao kwa hiari yao, wameyakataa mapenzi yao wenyewe na wamekuja kuyajua Mapenzi Yako.

316 Hao watoto, Bwana, wengi wao wakiwa ni watoto wachanga tu. Jinsi unavyowanyonyesha mikononi Mwako! Jinsi mama anavyomshughulikia mtoto wake, akiyapangusa machozi kutoka machoni mwao na—na kuwapa vitu maalum kwa kuwa anawapenda. Hivyo ndivyo unavyowapenda watoto Wako wachanga waliozaliwa karibuni, Bwana. Hawawezi kutembea bado, hata hawawezi kuzungumza. Jambo pekee wanaloweza kufanya ni kulia na kumtegemea Mama. Ee Mungu, washikilie mikononi Mwako, kwa upole, kama wana-kondoo wadogo, na uwaongoze mpaka watakapokomaa hata waweze kutembea. Kisha uwaongoze, Bwana, kupitia kwenye njia za utumishi. Tujalie.

317 Tusamehe dhambi zetu, kama sisi nasi tuwasameheavyo wale wanaotukosea. Usitutie majaribuni, bali utuokoe na uovu. Kwa kuwa Ufalme ni Wako, na nguvu, na utukufu, milele, kupitia Jina la Yesu Kristo. Amina.

318 Mungu awabariki! Ninatumaini ya kwamba Bwana amewafanyia jambo fulani asubuhi ya leo kuwafanya muanze Mwaka Mpya juu ya jambo hili moja, ya kwamba mnampenda Yesu Kristo, na siku moja mnataka kumwona na kumpenda na kuishi pamoja na Yeye milele. Ni shauku yangu kwamba hakuna mmoja wenu atakayepotea, ya kwamba kila mmoja wenu ataokolewa na kujazwa na Roho Mtakatifu, na kuhifadhiwa hata siku hiyo ya Kuja Kwake, kwa kuwa ninaamini ni hivi karibuni.

Sasa ninairudisha ibada kwa Ndugu Neville.

Ufunuo, Mlango Wa Nne Sehemu Ya II SWA61-0101
(Revelation, Chapter Four Part II)
Mfululizo wa Ufunuo Wa Yesu Kristo

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 1 Januari, 1961, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org